BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

Simu Nam. + 255 24 2230602/1
Fax Nam. + 255 24 2230215
Tovuti: www.zanzibarassembly.go.tz

SANDUKU LA BARUA 902,
ZANZIBAR
Barua Pepe: zahore@zanlink.com

ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

2016 - 2020

1.	**Mhe. Zubeir Ali Maulid**	**-**	**SPIKA**
2.	**Mhe. Mgeni Hassan Juma**	**-**	**Naibu Spika/ Nafasi za Wanawake**
3.	**Mhe. Shehe Hamad Mattar**	**-**	**Mwenyekiti wa Baraza/ Jimbo la Mgogoni**
4.	**Mhe. Mwanaasha Khamis Juma**	**-**	**Mwenyekiti wa Baraza/ Jimbo la Chukwani**
5.	**Mhe. Balozi Seif Ali Iddi**	**-**	**MBM/Makamu wa Pili wa Rais /Kiongozi wa Shughuli za Serikali/ Jimbo la Mahonda**
6.	**Mhe. Issa Haji Ussi Gavu**	**-**	**MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Chwaka**
7.	**Mhe. Haji Omar Kheri**	**-**	**MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi**

			ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ/ Jimbo la Tumbatu
8.	**Mhe. Haroun Ali Suleiman**	**-**	**MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora /Jimbo la Makunduchi**
9.	**Mhe. Mohammed Aboud Mohammed**	**-**	**MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais /Uteuzi wa Rais**
10.	**Mhe. Dkt. Khalid Salum Mohamed**	**-**	**MBM/Waziri wa Fedha na Mipango /Jimbo la Donge**
11.	**Mhe. Mahmoud Thabit Kombo**	**-**	**MBM/Waziri wa Habari, Utalii, na Mambo ya Kale/Jimbo la Kiembesamaki**
12.	**Mhe. Riziki Pembe Juma**	**-**	**MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali / Nafasi za Wanawake**
13.	**Mhe. Balozi Amina Salum Ali**	**-**	**MBM/Waziri wa Biashara, na Viwanda / Uteuzi wa Rais**
14.	**Mhe. Balozi Ali Abeid Karume**	**-**	**MBM/Waziri wa Vijana, Utamaduni, Sanaa na Michezo/ Uteuzi wa Rais**

15.	**Mhe. Rashid Ali Juma**	**-**	**MBM/Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi/ Jimbo la Amani**
16.	**Mhe. Hamad Rashid Mohamed**	**-**	**MBM/Waziri wa Afya / Uteuzi wa Rais**
17.	**Mhe. Maudline Cyrus Castico**	**-**	**MBM/Waziri wa Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto/ Uteuzi wa Rais**
18.	**Mhe. Salama Aboud Talib**	**-**	**MBM/Waziri wa Ardhi, Nyumba, Maji na Nishati / Nafasi za Wanawake**
19.	**Mhe. Sira Ubwa Mamboya**	**-**	**MBM/ Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji/ Uteuzi wa Rais**
20.	**Mhe. Juma Ali Khatib**	**-**	**MBM/ Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Uteuzi wa Rais**
21.	**Mhe. Said Soud Said**	**-**	**MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Uteuzi wa Rais**
22.	**Mhe. Khamis Juma Mwalim**	**-**	**Naibu Waziri, Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora/ Jimbo la Pangawe**
23.	**Mhe. Mihayo Juma N'hunga**	**-**	**Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi**

				ya Makamu wa Pili wa Rais /Jimbo la Mwera
24.	**Mhe.**	**Shamata Shaame Khamis**	**-**	**Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ/ Jimbo la Micheweni**
25.	**Mhe.**	**Harusi Said Suleiman**	**-**	**Naibu Waziri wa Afya/ Jimbo la Wete**
26.	**Mhe.**	**Mmanga Mjengo Mjawiri**	**-**	**Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali /Jimbo la Mkoani**
27.	**Mhe.**	**Mohamed Ahmada Salum**	**-**	**Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji/Jimbo la Malindi**
28.	**Mhe.**	**Chum Kombo Khamis**	**-**	**Naibu Waziri wa Habari, Utalii na Mambo ya Kale/ Nafasi za Wanawake**
29.	**Mhe.**	**Shadya Mohamed Suleiman**	**-**	**Naibu Waziri wa Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto/ Nafasi za Wanawake**
30.	**Mhe.**	**Lulu Msham Abdalla**	**-**	**Naibu Waziri wa Vijana, Utamaduni, Sanaa na Michezo/ Nafasi za Wanawake**
31.	**Mhe.**	**Juma Makungu Juma**	**-**	**Naibu Waziri wa Ardhi,**

			Nyumba , Maji na Nishati / Jimbo la Kijini
32.	**Mhe. Hassan Khamis Hafidh**	**-**	**Naibu Waziri wa Biashara, na Viwanda /Jimbo la Welezo**
33.	**Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi**	**-**	**Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi/ Jimbo la Mtopepo**
34.	**Mhe. Abdalla Ali Kombo**	**-**	**Jimbo la Mwanakwerekwe**
35.	**Mhe. Abdalla Maulid Diwani**	**-**	**Jimbo la Jang'ombe**
36.	**Mhe. Ali Khamis Bakar**	**-**	**Jimbo la Tumbe**
37.	**Mhe. Ali Salum Haji**	**-**	**Jimbo la Kwahani**
38.	**Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata)**	**-**	**Jimbo la Kijitoupele**
39.	**Mhe. Ahmada Yahya Abdulwakil**	**-**	**Uteuzi wa Rais**
40.	**Mhe. Ame Haji Ali**	**-**	**Jimbo la Nungwi**
41.	**Mhe. Amina Iddi Mabrouk**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
42.	**Mhe. Asha Abdalla Mussa**	**-**	**Jimbo la Kiwengwa**
43.	**Mhe. Bahati Khamis Kombo**	**-**	**Jimbo la Chambani**
44.	**Mhe. Bihindi Hamad Khamis**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
45.	**Mhe. Hamad Abdalla Rashid**	**-**	**Jimbo la Wawi**
46.	**Mhe. Hamida Abdalla Issa**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
47.	**Mhe. Hamza Hassan Juma**	**-**	**Jimbo la Shaurimoyo**
48.	**Mhe. Hidaya Ali Makame**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
49.	**Mhe. Hussein Ibrahim Makungu (Bhaa)**	**-**	**Jimbo la Mtoni**

50.	**Mhe.**	**Jaku Hashim Ayoub**	**-**	**Jimbo la Paje**
51.	**Mhe.**	**Khadija Omar Kibano**	**-**	**Jimbo la Mtambwe**
52.	**Mhe.**	**Machano Othman Said**	**-**	**Jimbo la Mfenesini**
53.	**Mhe.**	**Makame Said Juma**	**-**	**Jimbo la Kojani**
54.	**Mhe.**	**Maryam Thani Juma**	**-**	**Jimbo la Gando**
55.	**Mhe.**	**Masoud Abrahman Masoud**	**-**	**Jimbo la Bububu**
56.	**Mhe.**	**Miraji Khamis Mussa**	**-**	**Jimbo la Chumbuni**
57.	**Mhe.**	**Moh'd Mgaza Jecha**	**-**	**Jimbo la Mtambile**
58.	**Mhe.**	**Mohamed Said Mohamed**	**-**	**Jimbo la Mpendae**
59.	**Mhe.**	**Mohammedraza Hassanaali Mohamedali**	**-**	**Jimbo la Uzini**
60.	**Mhe.**	**Mtumwa Peya Yussuf**	**-**	**Jimbo la Bumbwini**
61.	**Mhe.**	**Mtumwa Suleiman Makame**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
62.	**Mhe.**	**Mussa Ali Mussa**	**-**	**Jimbo la Ole**
63.	**Mhe.**	**Mussa Foum Mussa**	**-**	**Jimbo la Kiwani**
64.	**Mhe.**	**Mwanaidi Kassim Mussa**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
65.	**Mhe.**	**Mwantatu Mbaraka Khamis**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
66.	**Mhe.**	**Dkt Mwinyihaji Makame Mwadini**	**-**	**Jimbo la Dimani**
67.	**Mhe.**	**Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy**	**-**	**Jimbo la Chaani**
68.	**Mhe.**	**Nassor Salim Ali**	**-**	**Jimbo la Kikwajuni**
69.	**Mhe.**	**Omar Seif Abeid**	**-**	**Jimbo la Konde**
70.	**Mhe.**	**Panya Ali Abdalla**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
71.	**Mhe.**	**Rashid Makame Shamsi**	**-**	**Jimbo la Magomeni**

72.	**Mhe.**	**Saada Ramadhan Mwendwa**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
73.	**Mhe.**	**Said Omar Said**	**-**	**Jimbo la Wingwi**
74.	**Mhe.**	**Said Hassan Said**	**-**	**Mwanasheria Mkuu**
75.	**Mhe.**	**Salha Mohamed Mwinjuma**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
76.	**Mhe.**	**Salma Mussa Bilal**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
77.	**Mhe.**	**Shaib Said Ali**	**-**	**Jimbo la Chonga**
78.	**Mhe.**	**Simai Mohammed Said**	**-**	**Jimbo la Tunguu**
79.	**Mhe.**	**Suleiman Makame Ali**	**-**	**Jimbo la Ziwani**
80.	**Mhe.**	**Suleiman Sarahan Said**	**-**	**Jimbo la Chakechake**
81.	**Mhe.**	**Tatu Mohamed Ussi**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
82.	**Mhe.**	**Ussi Yahya Haji**	**-**	**Jimbo la Mkwajuni**
83.	**Mhe.**	**Viwe Khamis Abdalla**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
84.	**Mhe.**	**Wanu Hafidh Ameir**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
85.	**Mhe.**	**Yussuf Hassan Iddi**	**-**	**Jimbo la Fuoni**
86.	**Mhe.**	**Zaina Abdalla Salum**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
87.	**Mhe.**	**Zulfa Mmaka Omar**	**-**	**Nafasi za Wanawake**

Ndg. Raya Issa Msellem - Katibu

Kikao cha Nane – Tarehe 18 Mei, 2018

(Kikao kilianza Saa 3:00 asubuhi)

DUA

Mhe. Spika (Zubeir Ali Maulid) alisoma dua

HATI ZA KUWSILISHA MEZANI

Waziri wa Habari, Utalii na Mambo ya Kale: *Bismillah Rahmani Rahim* Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba sasa kuwasilisha Hati Mezani ya Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Habari, Utalii na Mambo ya Kale kwa Mwaka 2018/2019. Naomba kuwasilisha Mhe. Spika.

Mhe. Ali Suleiman Ali: (Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake, Habari na Utalii): Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kuweka Hati Mezani Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Maendeleo ya Wanawake, Habari na Utalii Kuhusu Makadirio na Mapato na Matumizi ya Wizara ya Habari, Utalii na Mambo ya Kale kwa Mwaka 2018/2019. Naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2018 - 2019
Afisi ya Rais Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora

(Majadiliano yanaendelea)

TAARIFA

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Spika, kwanza nikushukuru nimesimamia Kanuni ya 45 sijui kama utaniruhusu niisome au muda utakuwa muafaka utaikubali ambayo inafatiwa na Kanuni ya 46.

Mhe. Spika: Isome

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Spika, 45

> "Mjumbe yoyote anaweza kuwa kibali cha Mhe. Spika, kutoa maelezo yake binafsi wakati unafaa kufuatana na mpangilio wa shughuli ambazo unawekwa kwa Kanuni".

Mhe. Spika, maelezo binafsi sikufahamika vizuri jana na hivyo nataka kuweka *Hansard* sawa lakini vile vile pana ya 46 ndio kubwa zaidi kama utaniruhusu au tusipoteze muda niiache nayo.

Mhe. Spika: Sijakufahamu Mheshimiwa.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Baada ya hiyo ya 45 kuna Kanuni ya Nam. 46 mbele yake

Mhe. Spika: Ndio nimeshafahamu kuhusu Kanuni sijafahamu hilo tatizo lako.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Spika, jana kiti chako kupitia Naibu Spika, sio wewe nafikiri na tulikuwa tunapigia kelele sana suala hili la *ecco* ndani na sifikirii Mhe. Naibu Spika, kutenda kitendo kama hicho, lakini baada ya kumuuliza akanambia *ecco* alisikia lugha nyengine na kuweka *hansard* sawa hapa limetajwa neno kunyanyasika sikusema Serikali hii inanyanyasika na *hansard* ninazo, naomba nikuletee *copy* moja upate kuona kama ni ushahidi.

Mhe. Spika: Mhe. Jaku nadhani nimekuelewa ulichokuwa unajaribu kukifanya ni kurekebisha tu hiyo *hansard* kama ilivyokuwa hapo awali ambapo unasema ulikuwa hukufahamika, mie nadhani haya masuala yafike pahali basi yawe yamekwisha. *hansard* itazingatiwa kama hivyo ulivyokuwa umesema wewe hapo awali kwa hiyo nafikiri liwe limeishia hapo ili tusiendeleze tena haya malumbano kwa sababu kwanza tuna tatizo la wakati, nadhani umenielewa. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wajumbe leo ni siku ya Ijumaa na Ijumaa ya mwanzo ya ndani ya mwezi wa Ramadhani mwisho wa shughuli zetu itakuwa saa 6:00 na kama mtaangalia *Order paper* mtagundua kwamba hata maswali tumeyaondosha na tumeyaondosha kwa maana ya kutaka kujaribu kuokoa huu wakati, kakini pamoja na hivyo kulikuwa na wachangiaji walikuwa wamebaki naona kuna majina manne nilikuwa ninayo hapa Mhe. Ali Khamis Bakari, Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy, Mhe. Waziri Said Soud pamoja na Mhe. Mwenyekiti Mwanaasha Khamis Juma nashawishika sana kwanza majina haya niyakate kwamba nisiwape nafasi ya kuchangia ili huu wakati tulionao tusifike pahali tukataka tena kuongeza muda baada ya saa sita (6). *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, kabla hajazungumza Mhe. Waziri mwenyewe mtowa hoja nitawapa watu wawili (2) kwanza nitampa Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu halafu nitampa Mheshimiwa Naibu Waziri wa hii Wizara baada ya hapo nitamwita mtowa Hoja ili aweze sasa kujibu na kutoa maelezo yale ambayo mlikuwa mnayachangia tokea jana, baada hapo sasa naomba nimwite Mwanasheria Mkuu ili sasa nae aweze kutoa mchango wake, karibu sana.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi kusema machache katika hoja hii ambayo iko mezani ya Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora ya Makadirio na Matumizi ya Ofisi yake kwa Mwaka wa fedha wa 2018/2019.

Mhe. Spika, awali ya yote naomba nichukuwe fursa hii kutoa shukurani kwa Mwenyezi Mungu *Subhana Wataala* kwa kutujaalia leo ni siku yetu ya pili katika mfungo wetu huu wa Ramadhani. Kwa namna hiyo naomba nichukuwe nafasi kwanza kabisa kumuombea Ramadhani Kareem Kiongozi wetu wa Nchi Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi pamoja na familia yake yote lakini pia nikuombee wewe Mhe. Spika, pamoja na wajumbe wote na wananchi wote wa Zanzibar Mwezi Mtukufu wa Ramadhani na pale ambapo tuliteleza kwa namna yoyote katika miezi 11 iliyopita basi hii ndio fursa ya kufutafuta na kujiweka sawa.

Mhe. Spika, baada ya hayo, nichukuwe fursa hii kumshukuru sana Mhe. Waziri kwa ushirikiano ambao amekuwa akitupa tokea apewe dhamana hii kuiongoza hii Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora na tumekuwa tukifanya kazi vizuri naomba nimuhakikishie Mhe. Spika, kama tutaendelea kumsaidia katika kutimiza majukumu yake aliyopewa ili wizara hii itapofika 2020 iwe ni mfano wa wizara katika mambo ya Sheria, Katiba na Utawala Bora tutaendelea kumsaidia na tunajuwa ananguvu za Mhe. Rais katika kutimiza hayo.

Mhe. Spika, kwa sababu ya muda na kama ulivyosema leo ni Ijumaa basi na mimi nitakwenda haraka haraka ili kumsaidia Mhe. Waziri kwenye baadhi ya ufafanuzi ambao Waheshimiwa Wajumbe wameyazungumza jana. Kwanza nitazungumzia yale ambayo kwenye fungu langu ambalo ni (G03) na kwa sababu na mimi niko hapa naomba niwaombe Waheshimiwa Wajumbe kama watupitishie fungu hili ili tuendelee na kazi ya kutimiza wajibu wetu kama ambavyo tumepewa na Katiba na Sheria mbali mbali.

Mhe. Spika, mbali ya yale ambayo tumeyaeleza ndani ya hotuba yetu kuna mambo ambayo tumeyafanya hayakuwemo ndani ya hotuba, nadhani ni muhimu kwa Waheshimiwa Wajumbe na Wananchi kuyajua. Moja halikujitokeza vizuri, suala zima la siku yetu ya Sheria *load A* imeshakuwa sasa ni mwaka wa 8 tunasherehekea siku ya Sheria lakini haikutoka vizuri kwenye vitabu vyetu. Nadhani kuanzia mwakani tutajitahidi kuhakikisha kama tunaelezea vizuri *activity* nzima ambazo tumekuwa tunafanya katika siku hii ya sheria.

Mhe. Spika, lakini kwa upande wetu tuliweza kutumia siku hii ya sheria kwa mwaka huu kufanya *out rich programme,* tuliamua kufunga ofisi zetu mjini na kwenda kwa wananchi. tulipeleka huduma zetu kwa wananchi. Niwashukuru sana wananchi, walitupokea vizuri na kimsingi walituhoji kama kwa nini mda mrefu tumetumia bila ya kupeleka huduma zetu kwao na wao wanahitaji msaada wa kisheria. Kwa hivyo niwaahidi wananchi kwamba kuanzia mwaka huu wa fedha huo ndio utakuwa utamaduni na utaratibu wa kazi wa ofisi yetu kwa kadri hali itavyokuwa kwa mwaka mara 1 au mara 2 tutakuwa tukifanya *out rich programme* na kupeleka huduma zetu kwa wananchi, ili kusikiliza matatizo yao ya kisheria na kuwasaidia pale ambapo itawezekana. Niwaombe sana wananchi wawe tayari kutupokea kama ambavyo wemetupokea katika kipindi hichi cha mwaka huu wa fedha ambapo tulianza kufanya *programme* hiyo.

Lakini ya pili Mhe. Spika, pia niliweza kukaa na kukutana na wenyeviti wa Bodi ya Wakandarasi, Wenyeviti wa Bodi ya Uhandisi na Taasisi zote ambazo zinahusika na usajili wa Kandarasi ili kulizungumza kwa pamoja suala zima hili la usimamizi hasa wa majengo ya serikali inapofika kwenye usimamizi wa mikataba. Waheshimiwa Wajumbe wamekuwa wakituhimiza sana kulitizama kwa jicho la pekee suala hili la usimamizi wa mikataba, naomba nichukuwe fursa hii kuwahakikishia Waheshimiwa Wajumbe kama suala hili sasa tumelipa namna yake pekee ya umuhimu katika kulisimamia na tumeamua kuunda timu rasmi sio tu ambayo itakuwa inaongozwa na Wanasheria lakini itajumuisha wataalamu kutoka Taasisi zote ambao ni Wahandisi, Wakadiriaji Majengo, na wale wote ambao wanataaluma hii katika fani ya ujenzi.

Mhe. Spika, tumegundua kwa kipindi kirefu tumekuwa tukizingatia mikataba kwa kutizama utaratibu wa kisheria, lakini kwa sababu ya ukosefu wa fani hizi za ujenzi pale katika ofisi yetu tumekuwa hatupigi jicho sana kwenye maeneo hayo, kwa sasa tumeamua tutakuwa tunawashirikisha hasa taasisi yetu ya Wakala wa Majengo ya Serikali ili kuhakikisha wanatusaidia katika fani hii na kuhakikisha *programme* zote ambazo zilipangwa na serikali zinatimizwa vizuri. Hivyo niwahakikishie Waheshimiwa Wajumbe kama kuanzia mwaka huu wa fedha suala hili la usimamizi wa majengo ya serikali kwenye mikataba hii itakuwa inasimamiwa vizuri na tutaunda Kamati Maluum ambayo itajumuisha Wanasheria na Wataalamu wote hao ambao nimewataja ili sasa tuweze kulisimamia vizuri. Niwaombe pia Waheshimiwa Wajumbe kama na wao wanaopitisha haya mafungu katika Kamati wahahakikishe kama wanapokwenda kwenye hizi ziara wanahoji taasisi na wizara ambazo zimeingia kwenye hii mikataba ili kuhakikisha kama mikataba ile inasimamiwa vizuri. Tukimaliza kwenye suala hili la mikataba tutaingia kwenye suala la ujenzi wa barabara kwa kusaidiana na Mhe. Waziri, maana nayo malalamiko yamekuwa mengi kwamba masika hadi masika barabara zinabomoka.

Sasa na hili niwahakikishie Waheshimiwa Wajumbe kama na hili tutalisimamia, tutahakikisha pia tunaunda timu ya kutushauri vizuri ya namna gani usimamizi wetu huu wa barabara tuusimamie vizuri na hasa aina ya lami ambazo zinatakiwa kuletwa nchini. Wajumbe wawe na imani kama kuanzia mwaka huu wa fedha masuala haya tutayasimamia vizuri na kwa kasi zaidi ili tija ile inayotakiwa kupatikana iweze kupatikana.

Mhe. Spika, Waheshimiwa Wajumbe wengi walizungumzia suala la ucheleweshaji wa kesi hasa kutoka Ofisi ya DPP na kwenda Mahakamani na Mahakama kutoa hukumu. Naomba niwakumbushe Waheshimiwa Wajumbe kifungu cha 12(6)(i) cha Katiba yetu ya Zanzibar ambacho kinasema kwamba.

"Kesi za jinai zitasikilizwa na hukumu yake kutolewa kwa haraka"

Mhe. Spika, kwa nini Katiba imeweka kifungu hicho? Kwa sababu Katiba inataka kuhakikisha yule ambaye ametuhumiwa basi anajua hatma yake mapema, kwa sababu kwenye kesi hizi za jina kuna adhabu mbali mbali na adhabu ya juu kabisa ambayo mtu anatakiwa ni kutiwa kitanzi hadi kufa. Sasa si vizuri kumuweka mtu akiwa hajijuwi khatma yake ni nini. Anatakiwa ajuwe khatma yake haraka kwa kusikilizwa kesi yake kwa haraka na maamuzi ya kesi ile kutolewa kwa haraka. Sasa kwa kutambua umuhimu huo nimshukuru sana Mhe. Jaji Mkuu wa Zanzibar Mhe. Omar Othman Makungu ametoa *circular* Nam. 1 ya mwaka 2018 nadhani nitamuomba Mhe. Waziri kama ikiwezekana nayo hii awapatie kila mjumbe *circular* hii Nam. 1 ya mwaka 2018, ndani ya *circular* hii umeelezwa utaratibu mzima kuanzia pale kesi inapofunguliwa mpaka pale hukumu inapotakiwa kutolewa na siku zake zimeelezwa kama Jaji akipokea kesi *file* anatakiwa kwa muda fulani afanye nini na muda afanye nini. Niwahakikishie Waheshimiwa Wajumbe kama suala hili ndio kwanza limeanza kutumika na *circular* hii imetolewa tarehe 12 Februari, 2018. Sasa ndio kwanza inaanza kutumika lakini itakuwa vizuri kila Mheshimiwa Mjumbe nae akawa nayo *copy* yake ili nae ajuwe nini kimo ndani ya *circular* hii.

Mhe. Spika, hayo ni kwa upande wa Mahkama lakini kwa taasisi zetu bado pia tunajukumu la kuhakikisha tunaiga mfano ambao umetolewa na Mahkama ya kuhakikisha kwamba pale ambapo tunapokea majalada basi na sisi tunajiwekea muda maaluma wa kuhakikisha kwamba

majalada haya tunayaondoa ndani ya mikono yetu. Kwenye hili niwahakikishie Waheshimiwa Wajumbe kama na hili pia tutalisimamia vizuri kwa kadiri ya uwezo wetu.
Mhe. Spika, ni mshukuru sana Mhe. Ali Suleiman Ali alituhimiza juu ya namna ya kuwajiri wataalamu na kusomesha wataalamu zaidi kwenye fanii hii ya kisheria nimewaahidi kama hiyo ndio azma na kupitia bajeti hii nishukuru sana Wizara ya Fedha imetupatia bajeti ya kutosha basi tutajitahidi sana sana kuhakikisha ndani ya ofisi yetu ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, lakini na ndani ya taasisi hizi za wizara basi tunasomesha hawa wanasheria kwenye fani maalum ambazo zitatusaidia katika nchi yetu fani zenyewe kama mafuta na gesi, na utaalamu huu wa kwenye majengo na fani mbali mbali ili kuhakikisha kama tunapata wanasheria wenye taaluma na waliobobea katika fani tofauti. *(Makofi)*

Mhe. Spika, Mhe. Suleiman Sarahani Said yeye alisema mambo mengi na katika mambo ambayo aliyasema moja alitaka kujua tofauti ya Jela na Chuo cha Mafunzo anadhani sasa kumekuwa tena hakuna Chuo cha Mafunzo na wanafunzi wale wamekuwa wanapelekwa jela. Nimhakikishie Mhe. Suleiman Sarahani Said kama bado sheria yetu Nam. 1 ya mwaka 1980 inakitambua Chuo cha Mafunzo kama ni Chuo cha Mafunzo na sio jela na kama Mhe. Suleiman Sarahani akipata nafasi ya kuisoma sheria hiyo basi aanze kusoma Kifungu cha 3 cha sheria hiyo ambayo ndio kinaanzisha hiyo Idara Maalum itayojulikana kama Chuo cha Mafunzo.

Mhe. Spika, Kifungu cha 4(2) cha sheria hiyo kinaeleza dhamira ya kuanzisha chuo hicho ni kuwasaidia wanafunzi ambao wanapelekwa pale ili kuwarudisha wawe ni watu wazuri katika jamii. Katika kufanya hilo sheria imeweka mafunzo ambayo yanatakiwa wapewe wanafunzi hao ikiwemo mambo ya kilimo, ikiwemo ufugaji, kazi za ujenzi, na kazi nyingi zimeelezwa ndani ya sheria hiyo. Nimhakikishie Mhe. Suleiman Sarahani Said kama inawezekana kwa uwezo wetu wa serikali bado hatujaweza kwa namna kubwa kuweza kufanikisha mambo haya. Lakini kwa kadri ya uwezo wa bajeti itavyokuwa tutazidi kuyasimamia mambo haya, sasa awe na amani kwamba bado chuo kile kinaitwa ni Chuo cha Mafunzo. Nimuhakikishie tena kwamba serikali katika kuhakikisha haiwatesi wanafunzi ambao wanapelekwa pale Zanzibar imekuwa miongoni mwa nchi moja za kwanza kuondoa adhabu za viboko. Kama unakumbuka zamani ilikuwa ukipelekwa ndani mbali ya kupigwa adhabu ya jela lakini pia unapigwa na adhabu ya viboko. Mwalimu Nyerere mara nyingi anaoneshwa kwenye televisheni akielezea wale ambao walikuwa wanakula rushwa, akipelekwa ndani anapigwa viboko 12 na anasema akitoka anapigwa nyengine 12 ili akapate kumuonesha mke wake. Sasa sisi hapa tumeondoa utaratibu huo wa adhabu na hata kwenye sheria zetu nyingi ambazo tunazitunga adhabu ya kifungo au itakuwa adhabu ya faini, hakuna hizi adhabu nyengine ambazo zimewekwa.

Mhe. Spika: Mheshimiwa umebakiwa na dakika tatu.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Haya nitakwenda mbio mbio Mhe. Spika. Mengine ambayo amesema labda niseme hili ambalo amelisema Mhe. Rashid Makame Shamsi, kwanza ni hoja yake ya wanasheria ambao wameajiriwa serikalini na wamekuwa wakifanya kazi za binafsi na kuwakilisha watu binafsi dhidi ya serikali.

Mhe. Spika, nimhakikishie kwamba suala hili tutalisimamia na hawa wote ambao wanashughulika na biashara hii tutashughulika nao. Lakini alizungumzia kwamba, kwenye kitabu hiki cha hotuba ya Mhe. Rais hakuona kiambatanisho kilichoelezea kanuni zilizokuwemo

zilizofanyiwa kazi na Ofisi ya Mwanasheia Mkuu. Nimhakikishie kuwa kulikuwa na kiambatanisho Nam. 'B' ambacho kilieleza kanuni 12 ambazo tumezifanyia kazi. Najua yeye kwa nafasi yake ya Mwenyekiti wa Kamati ya Sheria Ndogo Ndogo alikuwa na hamu ya kujua sheria ndogo ndogo ambazo zimetungwa, ili kamati yake ikianza kufanya kazi basi ajue namna pa kupita. Basi nimhakikishie nitamuwasilishia hii orodha ili awe nayo na imrahisishie katika kutimiza majukumu yake.

Jengine haraka haraka ni lile ambalo alilisema Mhe. Hamza Hassan Juma. Mheshimiwa yeye alisema mawili, moja ni sheria ile ya utawala. Nadhani hili kwenye Kamati yetu ya Uongozi tumelizungumza vizuri halina haja ya kulitolea ufafanuzi tumefika pazuri.

La pili, Mhe. Hamza alizungumzia stahiki ambazo wanatakiwa wapewe hawa Mahakimu wa Mahakama ya Ardhi. Nimwambie Mheshimiwa kwamba Mahakimu hawa wanafanya kazi kwa mujibu wa sheria Nam.7 ya mwaka 1994 ndio inayoanzisha Mahakama ya Ardhi. Kwenye kifungu cha 5 cha sheria hiyo kinaeleza kuwa, Mwenyekiti wa Mahakama ya Ardhi au Naibu wake, au Hakimu mwenigne yeyote wa Mahakama ile atakuwa anapokea stahiki na mshahara kama ule ambao anapokea Hakimu wa Mahakama ya Mkoa. Hizo ndio stahiki ambazo zimewekwa kisheria, sasa kama Mhe. Hamza ana mawazo mengine zaidi ya haya ambayo yamewekwa kisheria basi awasiliane na waziri ili tujue namna gani tunaweza kuyafanyia kazi haya.

Mhe. Spika, lakini kiujumla niwashukuru sana Waheshimiwa Wajumbe ambao wamechangia hoja hii na mimi nimhakikishie Mhe. Waziri kama tutaendelea kumsaidia katika kutimiza majukumu yake na niishukuru sana kamati yetu ambayo inamaliza muda wake, niwaombee kama waendelee kurudi kwenye kamati hii ili tuendelee kufanya nao kazi kwa pamoja.

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo naiunga mkono hoja hii ya Mhe. Waziri kwa asilimia mia moja. Nakushukuru sana Mhe. Spika. *(Makofi)*

UTARATIBU

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy: Mhe. Spika, naomba kidogo nieleze.

Mhe. Spika: Tatizo nini?

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Alwardy: Tatizo kanuni ya 45 na 46. Mhe. Spika, tupo hapa kwa ajili ya wananchi na muda tunao wa kutosha, Ramadhani tungerudi hata saa nane baada ya sala tukaenda mpaka saa 11:00. Wajumbe waliokuwepo ni kidogo tuna mambo muhimu ya kuzungumza kwenye kamati hii.

Mhe. Spika: Mheshimiwa naomba tuendelee.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi (OR) Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Spika, nami nianze kumshukuru Mwenyezi Mungu *Allah SubnanaWataala* kunijaalia leo hii kuwa mzima na kupata fursa ya kuchangia hotuba hii ya Waziri wa Nchi (OR) Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Mwaka wa

Fedha 2018/2019, kwa njia ya kutoa ufafanuzi kwa baadhi ya michango na hoja mbali mbali ambazo ziliibuka kwa Waheshimiwa Wawakilishi walipokuwa wakichangia hotuba hii.

Mhe. Spika, nianze moja kwa moja...

Mhe. Spika: Waheshimiwa naomba tusikilizane, Mhe. Naibu Waziri endelea tafadhali.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Spika, niendelee moja kwa moja katika hoja iliyotolewa na baadhi ya wajumbe kuhusiana na suala zima la Kamisheni kwamba iandae taratibu maalum za ufuatiliaji, utekelezaji wa sheria na kanuni na taratibu za utumishi wa umma.

Mhe. Spika, ni kwamba Kamisheni ya Utumishi wa Umma suala hilo linaendelea kulifanya na imekuwa ikifanya ziara nyingi katika taasisi mbali mbali, mawizara na baadae kutoa ripoti na pale wanapokwenda wanapokuta zile kasoro basi huwa wanaelekeza ili kasoro zile zisiweze kutokezea katika siku zijazo.

Mhe. Spika, vile vile wajumbe walitaka kujua idadi ya watumishi waliotenda makosa ya kinidhamu na hatua zilizochukuliwa kwa mwaka wa fedha 2017/2018. Jumla ya watumishi 98 walitenda makosa ya kinidhamu na kuchukuliwa hatua za kinidhamu ikiwa 44 walifukuzwa kazi, 46 walipewa onyo lakini vile vile wawili kusimamishwa kazi.

Mhe. Spika, wajumbe pia walikuwa na hoja ya ushauri kuhusiana na ofisi yetu inayoshughulika na masuala ya kupambana na rushwa. Walikuwa wanazungumzia kwamba *ZAECA* haina usafiri wa kutosha ili kuhakikisha kwamba inafanya kazi yake vizuri na kuleta ufanisi na lile lengo lililokusudiwa kutekelezeka.

Mhe. Spika, ni kweli tunakiri kwamba ofisi hii kwa hivi sasa usafiri ambao upo sio wa kutosha, lakini serikali tunaendelea kufanya harakati na jitihada za makusudi kuhakikisha kwamba *ZAECA* wanapata gari za kutosha ili kazi zao ziende kama vile ambavyo tulivyokusudia.

Sambamba na hilo Mhe. Spika, mjumbe mwengine Mhe. Ali Suleiman Ali alieleza kwamba, hawa *ZAECA* mara nyingi huwa wanaandama wanasiasa wakati wa kipindi cha uchaguzi. Mheshimiwa nimjuilishe Mhe. Mwakilishi kwamba, *ZAECA* ipo pale kwa ajili ya kufanya kazi yake bila ya kujali ni aina gani ya mtu ana hadhi gani au anatokea chama gani. Kwa hivyo, *ZAECA* inapofanya kazi yake na inapoonekana kwamba kuna baadhi ya wanasiasa wamekamatwa na taasisi hii katika kutekeleza kazi zake isionekane kwamba inawaandama wanasiasa tu. Lakini ni vyema nitoe wito kwa wananchi kwa jumla kuwa *ZAECA* itahakikisha kwamba suala la rushwa linaondolewa au linapunguzwa kwa kiasi kikubwa nchini na wananchi pamoja na Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, tuhakikishe kwamba tunawapa elimu wananchi wetu namna gani ya hili tatizo ubaya wake ulivyo. Kwa sababu hata Mwenyezi Mungu pia amelikemea.

Kwa hivyo, niwaombe Waheshimiwa Wajumbe na sisi wenyewe tunapokuwa katika harakati za siasa basi tujitahidi kuepuka suala hili na tuseme *ZAECA* kama *ZAECA* tutahakikisha kwamba tunafanya kazi usiku na mchana na tunasema kwamba hatutomuonea haya mwanasiasa yeyote

katika cheo chake chochote na hakuna mtu yeyote atakayeturejesha nyuma kwa maslahi ya nchi yetu na kwa mujibu wa sheria inayotuongoza.
Mhe. Spika, kulikuwa kuna ushauri mwengine ambao umetolewa na miongoni mwa waheshimiwa kuhusiana na mpango wa *E-Government* umefikia wapi. Mhe. Spika, napenda kueleza kwamba *E-Government* inaendelea kufanya kazi yake kama ilivyo na mambo mbali mbali tayari yameshafanyika. Kwa mfano, kuna mfumo wa malipo ya serikali umeimarishwa kwa kufikisha moja kwa moja katika taasisi husika badala ya kufuatwa Wizara ya Fedha kama ilivyo awali. Kwa hivyo, hayo ni maendeleo kwa maana ya kwamba *E-Government* inaendelea kufanya kazi zake kama ilivyojipangia.

Mhe. Spika, kama hilo halitoshi, mfumo wa mishahara pia umeandaliwa upya na umeongezewa udhibiti wa taarifa zake na unaruhusu kila taasisi sasa hivi kusimamia taarifa za maslahi za wafanyakazi wao. Pamoja na hayo, mfumo wa likizo na safari imeandaliwa kwa kushirikiana na kampuni ya *Microsoft*. Kwa hivyo, kiufupi kwamba *E-Government* inaendelea kufanya kazi yake na tutarajie mafanikio makubwa hivi karibuni.

Mhe. Spika, niendelee kuhusiana na shamba la Mfenesini nategemea ni Mhe. Machano Othman Said. Nimwambie tu Mheshimiwa kuhusu kadhia hii sisi tuko tayari kukutana na yeye na tuko tayari vile vile tupate muda tuweze kwenda kutembelea hiyo sehemu na vile vile tuweze kufikia suluhu ambayo itakuwa ni suluhu bora zaidi.

Mhe. Spika, kwa hayo machache nami niseme naunga mkono hotuba hii ya Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumiiz ya mwaka 2018/2019. Ahsante

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Waziri na ahsante kwa kutuokolea muda vile vile. Sasa naomba Waheshimiwa WAjumbe kwa heshima na taadhima nimwite mtoa hoja ili aje ajumuishe hoja yake. Mheshimiwa una sasa nzima ya majumuisho. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Spika, sikupata bahati mimi jana kuwekewa gilasi hapa na leo vile vile. lakini *Inshaallah* Mwenyezi Mungu atanisaidia sauti yangu itasikika vizuri.

Mhe. Spika, awali ya yote nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu *Subhana Wataala* kutujaalia kuamka salama na leo kufika hapa katika Baraza lako tukufu hili kwa ajili ya kukamilisha matakwa ya wananchi. Pia nichukue nafasi hii kuwashukuru sana Wajumbe wa Baraza lako la Wawakilishi ambao kwa njia mbali mbali wamechangia hotuba yetu hii. Kabla sijaendelea Mheshimiwa nianze kumshukuru sana Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dokta Ali Mohamed Shein kwa namna anavyotuongoza, anavyoiongoza nchi kwa uadilifu mkubwa sana. Lakini pia kwa namna anavyotusaidia sisi kama mawaziri wake katika masuala mbali mbali yanayohusiana na wizara zetu.

Vile vile namshukuru sana kwa uteuzi alioufanya hivi karibuni kwa kumchagua Mwenyekiti wa Bodi ya Mkaguzi na Mdhibiti wa Mahesabu (*CAG*) Mhe. Balozi Mohamed Ramia. Nimpongeze kwa kututeulia Mkurugenzi mpya wa chuo chetu cha *IPA. (Makofi)*

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba uniruhusu niwataje waliochangia kwanza halafu nitaendelea na majumuisho. Mchangiaji wa mwanzo kwa niaba ya kamati alikuwa ni:

1. Mhe. Suleiman Makame Ali
2. Mhe. Ali Suleiman Ali
3. Mhe. Suleiman Sarahan Said
4. Mhe. Simai Mohamed Said
5. Mhe. Rashid Makame Shamsi
6. Mhe. Hamza Hassan Juma
7. Mhe. Omar Seif Abeid
8. Mhe. Machano Othman Said
9. Mhe. Viwe Khamis Abdalla
10. Mhe. Shehe Hamad Mattar
11. Mhe. Panya Ali Abdalla
12. Mhe. Salha Mohamed Mwinjuma
13. Mhe. Salma Mussa Bilal
14. Mhe. Mwanasheria Mkuu
15. Mhe. Naibu Waziri wa Nchi (OR) Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora

Pia naomba niwashukuru waliochangia kwa maandishi wakiwemo:

1. Mhe. Mwantatu Mbarak Khamis
2. Mhe. Waziri wa Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto
3. Mhe. Nassor Salim Ali
4. Mhe. Shehe Hamad Mattar
5. Mhe. Naibu Waziri wa Afya
6. Mhe. Tatu Mohamed Ussi
7. Mhe. Mohamed Mgaza Jecha
8. Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekizi wa Baraza la Mapinduzi na
9. Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais.

Mhe. Spika, wewe ni shahidi tulipoingia kwenye Baraza hili mara baada ya uchaguzi wa mwaka 2016 Baraza la mwanzo wakati nikiwasilisha bajeti yangu hapa michango iliyotoka katika kipindi kile, mwaka uliofuata na mwaka huu ni tofauti kabisa. Nawashukuru sana na nawapongeza wajumbe kwa jinsi walivyochangia michango yao mbali mbali kwenye hotuba yetu. Mara ya mwanzo walinambia tunakupa muda ukajiimarishe zaidi kwenye mambo haya kwa sababu ni mpya. Mara ya pili nikachezea bakora nzuri sana hapa wakasema hapana sumile katika haya, lakini mwaka huu *Alhamdulillah* tumeteremka vizuri sana michango ilikuwa mizuri. Hii ni kuonesha kwamba wajumbe wameridhika na kazi ambazo tunazifanya. Nashukuru sana. *(Makofi)*

Mhe. Spika, Waheshimiwa waliochangia nawashukuru sana wote. Namshukuru sana Mwanasheria Mkuu amenisaidia sana masuala ya kisheria ya Mahakama na Mhe. Naibu Waziri wangu amechangia. Kwa hivyo, mimi kazi yangu itakuwa ndogo sana na pengine sitotumia muda mrefu ili kunusuru muda wako lakini pia tuweze kuwahi sala ya Ijumaa.

Mimi nitaanza kulizungumzia suala zima la Chuo cha Utumishi wa Umma (*IPA*). Bahati nzuri wajumbe wengi sana wamechangia eneo hili, sitotaja nani na nani kachangia lakini nataja kwa jumla tu ili kuokoa muda vile vile.

Mhe. Spika, Chuo cha Utumishi wa Umma kilianzishwa kisheria na kikiwa na madhumuni hasa ya kutoa mafunzo kwa ajili ya wafanyakazi watumishi wa serikali. Sasa tumekwenda kuanza kutoa cheti na baadae tukaanza kutoa diploma au stashahada. Sasa katika maendeleo ya ukuaji wa chuo kile ikafika wakati kwamba chuo kikaanza kufikiria kuanzisha *degree* ya kwanza na mwaka jana walitaka kuanza lakini haikuwezekana kuanza mwaka jana matayarisho yalikuwa bado hayajakamilika, wakasema tutajiandaa wakapewa muda, wizara na serikali ikawapa muda wajiandae zaidi, tukafika mahali wakaja *NACTE* na *TCU* kwa upande mmoja hasa *NACTE* wakaruhusu wakakitambua kile chuo kwa utaratibu ambao wanasomesha masomo yao na wana mashirikiano mazuri sana kati ya *NACTE* na *TCU*. Kwa hivyo, wale ambao walisema je, chuo hiki kinatambuliwa? Naam, chuo kinatambuliwa na *NACTE* na *TCU* bila ya matatizo yoyote na wanafunzi wasiwe na wasiwasi wowote vyeti vyao vinatambulika.

Sasa mwaka huu wakati wanaanza na *course* ile ya *degree* tukasema hiki chuo kinaanza na *degree* tayari kimeshawiva? Tukapeleka maombi yetu serikalini na serikali ikatushauri vizuri sana, ikasema hakuna matatizo mnaweza kuanza lakini wakati huo sasa itabidi iundwe timu ya kwenda kukagua chuo chetu cha *IPA*.

Mhe. Spika, timu imeundwa, imekwenda na imekuja ripoti nzuri sana, ripoti hiyo sio tu kama imeisaidia serikali lakini imeisaidia hata chuo chenyewe cha *IPA*. Tumefanya juhudi tumewaita *IPA*, tumewaelekeza vya kufanya. Sasa baadhi ya waheshimiwa wamesema tumesimamisha udahili wa wanafunzi, hatujasimamisha udahili wa wanafunzi kwa sababu wanafunzi wanasoma pale, wale walioanza na *degree* wanaendelea na watasoma mpaka watamaliza, isipokuwa *bench* ya pili ambayo ilikuwa ichukuliwe mwakani hiyo itachelewa kidogo kwa sababu kuna mambo lazima tuyarekebishe kwanza ili chuo kile kiwe na hadhi kubwa zaidi na kiwe na kila kinachohitajika kiwepo pale, hasa vitabu, vifaa na walimu wenye sifa zaidi kuliko wale ambao wapo pale. Lakini pia na miundombinu mbali mbali ambayo inahitajika kuwepo pale. Naomba sana sote tufahamu kwamba Chuo cha *IPA* kipo kwa ajili yetu, lakini tutazidi kutilia mkazo na tutaendelea kutoa mkazo kwamba chuo kile zaidi badala ya kuchukua wale *presurvice* kitachukua zaidi *insurvice* yaani wale waliokuwepo katika ofisi zetu mbali mbali. Natoa wito kwa mawaziri wote wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, wakurugenzi, makatibu wakuu na viongozi wote wawapeleke wafanyakazi wao pale wende wakapate mafunzo hasa wale ambao wamepata mafunzo ya muda mrefu na wale ambao hawajapata mafunzo ya aina yoyote, wende pale watapata mafunzo kwa ajili ya kuweza kujiimarisha katika shughuli za kiutumishi.

Mhe. Spika, nadhani suala la *IPA* nimelizungumza kwa kiasi kikubwa nadhani tufikie hapo.

Suala la pili ambalo napenda nilizungumze kidogo kuna suala zima la *ZAECA*. *ZAECA* waheshimiwa wamelalamika namshukuru Mhe. Naibu Waziri amelizungumza vizuri, kwamba inafuatilia zaidi viongozi wa CCM. Nasema hivi Mhe. Spika, *ZAECA* kamwe hawatowafuata viongozi wa CCM itamfuata mwananchi yeyote, kiongozi yeyote ambaye atakwenda kinyume na utaratibu. Tumeshajuilishwa rushwa na madhara yake, hicho kitabu cha bajeti hebu watizame kule kwenye gamba ukurasa wa nyuma kabisa, kuna nambari 113 aliizindua waziri huyo

aliyesimama mbele yenu ndiye aliyezindua nambari hiyo. Sasa hebu iaangalieni vizuri sana nambari hiyo, hiyo itatumika na imeanza kutumika na *Alhamdulillah* tumeshapata taarifa nzuri na tunaendelea kuzikushanya na zitafatiliwa zaidi nyendo mbali mbali, tizameni kwenye taarifa ya kitabu chetu cha bajeti jinsi gani *ZAECA* ilivyoweza kuoka pesa karibu milioni mia na moja na ushee hivi kwa ajili ya kupambana na masuala haya.

Hata kwenye tiketi za mpira pale watu huchukua rushwa zimekatamatwa vile vile, taarifa hizo zipo kwenye maeneo mengine vile vile. Kwa hivyo, tutaendelea tusishituke, usimuogope askari kama hujafanya kitu. Lakini ukimuogopa askari lazima kuna jambo utakuwa umelifanya. Kwa hivyo, Mhe. Spika, wasiogope tuendeleeni *inshaallah* tuingieni kwenye uchaguzi wetu kwa salama na amani kwa kufata taratibu na maadili ya uongozi na maadili ya chama chetu.

Vile vile nizungumze suala la *CAG*, Mdhibiti na Mkaguzi wa Mahesabu. Mhe. Spika, Mdhibiti na Mkaguzi wa Mahesabu ya Serikali Waheshimiwa wengi wamelalamika hapa wamelalamika kwa sababu wanasema ripoti zinachelewa Waheshimiwa tunasahau sana. Miaka ya nyuma tulikuwa tunakaa miaka sita saba hatupati ripoti hapa. Wale Waheshimiwa wa zamani watakumbuka tunakaa miaka saba miaka minane hatujapata ripoti. Kwa kweli kwa kiasi kikubwa amejitahidi sana na hivi sasa hata ripoti ya mwaka 2016/2017 naweza kusema ipo tayari tujitayarisheni na hiyo tutaletewa na *inshaallah* tukijaaliwa ripoti yetu itafika hapa Barazani tutakuja kuiona ili *PAC* ifanye kazi yake. (*Makofi*)

Mhe. Spika, *CAG* kwa nini wafanyakazi wamewaondosha na leo wanadai wafanyakazi wengine wakati wamewaondosha. Nasema uhamisho katika Utumishi wa Serikali ni jambo la kawaida. Hatuwezi kubakia sote katika maofisi yetu pale pale kama tunahitajika mahali pengine utakwenda kufanya kazi. Wengi wetu tuliokuwemo humu tulikuwa tunafanyakazi katika maofisi mbali mbali. Sasa je, tusikupe Uwakilishi, tusikupe Ubunge tukurejeshe kule kule ukihitahijika mahali kama chama wananchi wamekuhitajia nenda na kama serikali inakuhitajia katika eneo jengine ambalo utaleta utekelezaji mzuri zaidi basi utapewa uhamisho. Wengi walikuwa walimu humu ndani, kuna walimu walikuwa *SUZA* kuna walimu wanasomesha maeneo mbali mbali na mpaka sasa tunaendelea kuwateua, huyo Ndugu Mwinyi Talib ni dokta huyo sasa tumwache huko aliko aendelee tu wakati anaweza kwenda kuongoza chuo, hatuwezi kufanya kitu kama hicho. (*Makofi*)

Tutaendelea mimi nasema pale ambapo panahitajika kumuhamisha mtu kwa dharura kama hizo za kuhitajia kwa ajili ya kuleta manufaa ya taifa letu hayo yatakuwa wanaendelea. Lakini afisi hii ilikwama kwa kipindi kirefu hapa tulipitisha sheria ya marekebisho *miscellaneous* ambayo *AG* alikuja nayo. Alikuja nayo hapa marekebisho ya sheria mbali mbali ikiwemo sheria ile ya Mdhibiti na Mkaguzi wa Mahesabu, tukarekebisha kipengele kile cha Bodi ya *CAG* ilirekebishwa vipi. Kwa sababu bodi mwanzo kwenye ile sheria ya mwanzo haikusema watakaa kwa muda gani kwenye uongozi. Matokeo yake ikawa bodi inakwenda tu haina muda mpaka bodi ikajiondoa wenyewe kwa sababu muda ushakuwa mkubwa ikawa tena haifanyi kazi haipo. Muda ushamalizika ushakuwa mkubwa.

Sasa nashukuru na nampongeza sana Mhe. Rais wangu wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi tayari keshamteua Mwenyekiti Mhe. Mohamed Ramia Abdiwawa na huwezi kuteuwa wafanyakazi ukawapeleka kwenye ofisi ya *CAG* bila ridhaa ya bodi. Sasa bodi imeshaundwa,

Mwenyekiti, keshachaguliwa. Sasa kazi hii iliyobakia ni ya waziri kuteua Wajumbe kuingia kwenye Bodi ile ili waendelee kutekeleza majukumu yao. (*Makofi*)

Kwa hivyo, naomba Waheshimiwa watulie wafanye shughuli zao vizuri watushauri ipasavyo na sisi tutaendelea kushirikiana nao kwa hali na mali. Nasema tena Mhe. Spika, tumebadika sana katika michango yetu mwaka huu. Nashukuru Mhe. Spika, nikupongeze wewe mabadiliko haya yanatokana na jinsi ya sera na usimamizi wako ulivyokuwa mzuri humu ndani ya Baraza letu. (*Makofi*)

Mhe. Spika, kuna jambo limetokea jana na mimi mwanaadamu sikutolewa nyongo nataka niliseme kidogo. Nifahamishe dunia na leo ni Ijumaa watakwenda kusali Ijumaa na Imam atatoa hutba leo atasema "Nakuusieni pamoja na kuiusia nafsi yangu". Mtatolewa hutuba hiyo na leo mtaisikia nendeni msikitini kwa wale watakaopata nafasi kwenda msikitini *inshaallah* nendeni mtasikia hotuba hiyo. Lazima aliseme jambo jambo hilo na mimi najiusia nafasi yangu kwa sababu na mimi ni mwanaadamu sikukamilika. Lakini tuchunge sana matamko yetu tunayoyatoa humu Barazani, hichi ni chombo kikubwa sana hiki.

Chombo hichi kinasikilikana dunia nzima sasa hivi usimchukie mtu mpaka dunia, mpaka kifaranga cha kuku akaona kwamba wewe unamchukia mtu yule haifai na sisi ni waisilamu wengine na dini zetu vile vile. Kila mmoja amuheshimu mwenzake. Pana machungu yalitokea hapa tunakumbuka kipindi fulani kuna Mheshimiwa alichangia machungu yale bado wana CCM wanayo hayajasahaulika yalitamkwa maneno mazito hapa ndani sitaki hata kuyasema maana yake yanatia uchungu.

Kifungu cha 59 cha kanuni yetu (a) kinasema: Mambo ambayo yanakatazwa Mhe. Spika, tufungue kifungu cha 59(a) kinasema nini.

"Maneno ya matusi na kashfa hayafai"

Mhe. Abdalla Diwani nakuasa sana wewe ni mchanga sana kwenye siasa katika Baraza hili. Ni mchanga maana yake ni mchanga wa mchanga kweli. Mimi niko kwenye Baraza hili tokea mwaka 2000 mwaka wangu wa 18 na *inshaallah* namuomba Mwenyezi Mungu anijalie nimalize kwa salama na amani. Bado machungu yale wananchi wa Zanzibar wanayo.

Jana wakati akichangia kuhusu Msikiti wa Shurba Mhe. Spika alitoa tamko ambalo lilinikera mimi. Lakini pia wananchi wa Makunduchi wamekereka. Kwa nini awataje wananchi wa Jimbo la Makunduchi hapa. Awataje kwa njia za kheri kama hajui wananchi wa Jimbo la Jan'gombe na Makunduchi ni marafiki na yeye anajua hata wakitaka kuvunja SACOS zao, *JICA* zao wanakuja Makunduchi wanavunja kule kule, tena wanafikia nyumbani kwa huyo huyo Mwakilishi wa Makunduchi. Leo anatoa tamko hapa anasema kwamba msikiti ule ungekuwa uko Makunduchi basi lingekuwa tatizo lile limeshamalizika.

Si jambo zuri wala si jambo la hekima na busara, tujitahidini sana kuchunga midomo yetu tuna mengine tunayavumilia hapa, tukisema sisi wakati ni mawaziri tunaonekana ni watu wa ajabu na sisi ni binaadamu tunafika wakati lazima na sisi tuyaseme haya. (*Makofi*)

Tujirekebisheni Waheshimiwa sisi ni viongozi mimi humu Barazani nasema watu wote wanatuheshimu napata heshima kubwa humu ndani nashukuru sana nawashukuru wote na asilimia kubwa ya humu ndani ama ni wanafunzi wangu au pengine walisoma wakati mimi mwalimu tayari hawakusoma ile skuli niliyofundisha tu pengine wapo hapa. (*Makofi*)

Siku moja nilimtania mwanafunzi wangu Hamza Hassan Juma mwaka jana kila ninavyomfahamisha hafahamu na bahati nzuri bajeti zangu zote watu wengi hawapigii miguu tokea niko Wizara ya Elimu yeye atasimama apige mguu. Lakini mimi huwa sikereki ananipa changamoto kwa sababu hakuchangii kwa kunipa kashfa kunipakazia au pengine kunitukana au vipi anachangia *very constructively* nampongeza. (*Makofi*)

Nikamwambia Hamza nilifundisha darasani hukufahamu sasa nitakupeleka Elimu Mbadala, labda kule atafahamu zaidi nilimwambia yule pale yuko simsemi kwa sababu kama hayupo, yupo na wengine wapo wengi humu ndani. Sasa mimi kwa umri sasa hivi *Alhamdulillah* sitini naa. Sasa jitizameni, kuna maneno mkiyasema myapime unamwambia waziri, ukimwambia waziri unaiambia serikali. (*Makofi*)

Mimi sikuteuliwa kwa sababu ya jambo lolote kwa sababu Mwenyezi Mungu kataka na Rais wangu kapenda aniteuwe. Kwa imani aliyokuwa nayo kwetu sisi sote kwa sababu ya kukipenda Chama cha Mapinduzi na kuwapenda wale viongozi ambao wako tayari kuitumikia nchi na mimi ni mmoja wapo nimejitolea.

Mimi kwenye siasa sikulazimishwa Mhe. Spika, ni mwanachama toka *Afro Shirazy* na kadi ninayo mimi sikuchapia gari mimi. Inakuja CCM 1977 mimi tayari nina kadi ya *Afro Shirazy* zamani na mimi kadi yangu nnayo na nambari 0101012 ya CCM tena "A" 01 imeanza wakati ule katika wanachama wa mwanzo kabisa.(*Makofi*)

Sasa siwezi kupewa nafasi kama hizi kama sikuaminiwa kiasi hicho sijapatapo Mhe. Spika, sijapatapo kumbagua mtu sijui nitambagua nani nikimbagua mtu mimi nitabaguliwa vipi? Mimi nakipongeza sana Chama changu cha Mapinduzi hakina ubaguzi, Serikali ya CCM haina ubaguzi, Rais wangu hana ubaguzi. (*Makofi*)

Sasa tunapokuja hapa tukaanza kugawana mipaka tukaanza kugawana maeneo hatufiki jamani, wewe unamfikiria huyu sie basi pengine ndie kuliko wewe. Usimdhanie mtu kwa rangi yake kwa umbo lake, kwa dini ukaona hafai, jitizame wewe mwenywe. Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa aliyestaafu Koffi Annan alisema ukitaka kuangalia maendeleo sio kama vile unakwenda kwenye kiyoo unajitizama unajiona nafasi yako, kipaji na ukweli umo ndani ya nafsi ya mtu. (*Makofi*)

Mhe. Spika, samahani imebidi niseme leo kidogo hawajanisikia nikisema kama hivi watu wengi. Mimi ni mtu wa mas-hara ni mtu ambaye ni rafiki wa kila mmoja mkubwa mdogo hapa wote nawaheshimu lakini tuheshimiane basi na tuheshimiane. Wakati mwengine lugha zinazotoka humu ndani ndio yale yanavyotokezea humu ndani.(*Makofi*)

Kuna Mheshimiwa mmoja Mhe. Spika, wewe ulikuwa Waziri wa Mawasiliano wakati ule alinidhalilisha ndani Baraza akasema hivi:

Waziri uende Jimbo fulani silitaji maana nikilitaja mtalijua na huyu Mwakilishi alikuwa Upinzani bahati mbaya au bahati mzuri maana ni mpinzani. Akasema kwamba Waziri wende katika Jimbo langu ukawaombe radhi wananchi kwa sababu wewe uliwaahidi utawajengea madarasa manne ya skuli, wakati ule nilikuwa Waziri wa Elimu. Bahati nzuri Mwenyezi Mungu kanisaidia mimi wakati ule kabla sijasoma bajeti yangu huwa natembelea skuli zangu zote na maeneo yangu yote.

Kwa hivyo, nikifika kwenye Baraza najua kila kitu, wakati nafanya majumuisho kama haya nikamwambia Mheshimiwa nakuomba ukawaombe radhi wananchi wa Mkanyageni eee! wa Jimbo kuwasemea mambo ambayo hawajakutuma, kwa sababu mimi nimeshamaliza kazi ile inaonekana wewe hata jimboni kwako huendi. Maana yake ilikuwa kweli hajenda akanambia kweli sijapita samahani sana. Kwa hivyo, uombe radhi wewe sasa nisiombe radhi mimi, akaomba radhi Barazani pale.

Kwa hivyo, jamani tusemeni mambo haya tusaidiane kwa lengo la kusaidiana. Mimi sina tatizo nimemsamehe duniani na akhera mwenzangu huyu wala sina haja ya kuchukua hatua yoyote lakini nina nia nzuri. (*Makofi*)

Lakini suala hili la msikiti wa Shurba ni useme kidogo, Mheshimiwa kaja kule afisini kwangu mara ya kwanza mara ya pili. Tumechukuwa juhudi nimeita Afisi ya Mufti Shekh Thabit Nouman Jongo na wenzake wote nimewaita mbele yake na wazee alikuja nao na miongoni mwa wazee aliokuja nayo ambaye aliwahi kuwa Mwenyekiti wa Jimbo la Jan'gombe ambaye ni mtu wa Makunduchi vile vile hawa anaowasema, Mwenyekiti wa Jimbo la Jan'gombe alikuwa mtu wa Makunduchi. Lakini hapa hatuzungumzii Umakunduchi na Utumbatu na Unungwi hapa. Hapa tunazungumzia Uzanzibari. (*Makofi*)

Alipokuja, Mheshimiwa mimi nikamsaidia kwa nguvu zangu zote nikawaita Mashekhe tukaenda tukajadili, tukaandika barua Wizara ya Ardhi kuwaomba watupatie hati ili tuwakabidhi wenzetu. Juzi juzi Katibu Mkuu akatuandikia barua kwamba tunataka maoni yenu, maoni yetu sisi tunataka ipatikane hati wapewe wanaostahiki.

Lakini nataka nikwambie serikali haitaki kujiingiza kwenye mizozo ya dini, mizozo hii itatatuliwa huko huko na wananchi wenyewe ikiwa hapana budi Afisi yetu wa Mufti itasaidia. Lakini tujitahidini, masuala haya tukiyaleta Barazani ya kidini ugomvi ugomvi kama huo hautotusaidia tutayapalilia, tuko tayari kushirikiana wakati wote jambo hili likikwama la misikiti ni wajibu wetu sisi kama serikali tusaidie.

Lakini tusipendelee sana kila wakati tukawa tunaingia jikoni tunaingilia mambo haya maamuzi mazito ya kidini. Misikitini kuna taratibu zake na misikiti ina utaratibu mzuri wa heshima pale si pahali pa kugombana ile ni nyumba ya Mwenyezi Mungu, huwezi kwenda pale ukenda ukufanya mambo unayotaka mwenyewe ukawakataza wenzio wasisali, ukawakataza wenzio wasifanye hivi.

Kwa hivyo, tutajitahidi kadiri inavyowezekana mimi namuhakikishia Mhe. Abdalla Maulid Diwani bado suala hili lipo vizuri na tutajitahidi msikiti huu tuurejeshe mikononi mwenu kadiri itakavyowezekana ili watu waendelee kuutumia msikiti huu.

Mhe. Spika, baada hayo naona nisichukuwe muda zaidi michango yao tumeichukua, ushauri wao tumeuchukua na Mwenyezi Mungu akitujaalia *inshaallah* tutakwenda kutekeleza yote tuliyoambizana.

$$

MICHANGO YA MAANDISHI - WIZARA YA NCHI (OR) KATIBA, SHERIA, UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi (OR) Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora:

Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii (D12)

Wakala wa usajili wa matukio ya kijamii ni taasisi muhimu sana katika kuweka kumbukumbu mbali mbali zikiwemo kumbukumbu za usajili wa vizazi na vifo. Jitihada inabidi iongezeke katika kutoa elimu inayohusiana na usajili wa vizazi na vifo. Kuna baadhi ya wananchi huwa hawaoni umuhimu huo na hali hii hupelekea Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kukosa takwimu sahihi za vizazi na vifo nchini. Hali ni mbaya zaidi katika muitikio wa kusajili vifo vinavyotokea nchini, watu huwa hawajali kusajili vifo.

Jamii mara nyingi husajili vifo pale ambapo watu hao wanapohitaji kurithi mali za marehemu huyo. Kwa hivyo, ni vyema elimu ikaongezwa kutolewa ili wananchi waweze kusajili vizazi na vifo na ili serikali iweze kupata takwimu sahihi ya wananchi wake waliozaliwa na waliofariki, ili iweze kupanga mipango ya maendeleo vizuri zaidi.

Naunga mkono hotuba hii kwa asilimia mia moja. Ahsante.

Mhe. Tatu Mohamed Ussi: Mhe. Mwenyekiti, kwanza niipongeze Hotuba ya Waziri wa Nchi (OR) Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

Mhe. Waziri, G02 - Mahkama, ukurasa wa 23 kifungu cha 68. Nipongeze Mahkama zetu jinsi zinavyosimamia kesi katika Mahkama ya Watoto. Jumla ya mashauri 187 yameripotiwa, lakini mashauri yaliyosikilizwa na kutolewa uamuzi ni 44 tu. Kwa hivyo, mashauri yaliyobakia ni 143.

Mhe. Waziri, kutokana na hali hiyo, Mahkama hii inahitaji kuongeza kasi zaidi ya kusikiliza mashauri hayo ili kuondoa msongamano wa mashauri katika Mahkama hiyo.

Mhe. Waziri, G09 ukurasa wa 33 Tume ya Utumishi Serikalini. Tunapongeza Tume ya Utumishi Serikalini ni tume inayotoa ajira kwa vijana wetu, lakini pia napongeza kwa kuweka tathmini ya watumishi, lakini muda wa matangazo ya nafasi za kazi unakuwa mdogo. Lakini baada ya

matangazo na kufanya usaili matokeo ya usajili yanachelewa kutolewa. Hili linawavunja moyo vijana wetu na hatimae kukata tamaa ya kupata ajira.

Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana

Mhe. Waziri, nipongeze Kamisheni hii kwa kusimamia masuala ya Dini ya Kiislamu zikiwemo Sala na Mabaraza ya Iddi kitaifa, Hijja, Zakka na Misaada ya kheri.

Mhe. Waziri, naiomba taasisi hii kusimamia vizuri misaada ya kheri inayotolewa na Waislamu wenye nia njema ya kuwasaidia Waisilamu wenzao. Lakini kuna baadhi ya watu wanaopewa misaada hiyo haifiki kwa walengwa. Kwa hivyo, naiomba ofisi hii kuwaelimisha Maimamu na Misikiti au watu walioaminiwa basi sadaka hizi wazifikishe kwa walengwa, kwani kuna baadhi yao wakipewa misaada wanapeleka kwa jamaa zao tu.

Mhe. Waziri, baada ya mchango wangu huo naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

Mhe. Shehe Hamad Mattar: Mhe. Mwenyekiti, namuomba Mhe. Waziri anipe maelezo kuhusu mkataba wa Ofisi ya Wakfu na Mali ya Amana Pemba ambalo limejenga kwa mkataba wa kujilipa gharama kwa njia ya kodi, hadi fedha yake irudi. Nataka kujua mkataba huo unamalizika lini na kama unakaguliwa vyema.

Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi

Mhe. Mewnyekiti, afisi hii ni nyeti sana na kama itafanya kazi vizuri basi itaweza kuongeza ukuaji wa uchumi wetu kwa kusimamia viongozi ambao wanadhamiri ya uwekezaji hapa Zanzibar ambao ni vikwazo.

Pamoja na kutimiza masharti ya uwekezaji ya nchi lakini kama hajatoa chochote na wakati mwengine ameshatoa, lakini bado anasumbuliwa muda mrefu na hamaye kuamua kuondoka na kuwekeza nchi jirani ambapo kwetu ni hasara kwa uchumi ewtu.

Naomba sana taasisi yako itupie macho yao katika maeneo hayo na sio kwa watu wadogo tu. Naomba kuwasilisha.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Mwenyekiti, naipongeza hotuba ya Wizara hii ya Nchi (OR) Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Nampongeza Mhe. Waziri katika uwasilishaji mzuri, pia wafanyakazi wote kwa utendaji wao mzuri. Naanza kwa kuikumbusha Idara ya Mahkama kushughulikia kesi zilizoachwa muda mrefu zipitiwe ili zipatiwe ufumbuzi, kwani kuna malalamiko kwamba kuna kesi za zamani zimeganda na kesi za sasa zinapata hukumu.

Tume ya Utumishi Serikalini iangalie maslahi ya watendaji wa serikali zinachelewa sana, wafanyakazi vizuri basi wapatiwe maslahi yao. Naunga mkono asilimia mia moja ahsante.

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto: Napenda kupongeza juhudi za wizara yako wewe na watendaji wako wote kama na wewe ulivyowapongeza.

Mheshimiwa mimi naunga mkono hotuba yako kwa asilimia mia moja, lakini nina *observation* katika ukurasa wa 40 Programu ya Usimamizi wa Masuala ya Dini.

Napongeza ofisi yako kukamilisha muundo wa ofisi na kukamilisha idara na vitengo vyake ili vikidhi mahitaji ya jamii na viendane na teknolojia ya wakati tulionao. Aidha, kuimarisha shughuli za utoaji taaluma na dini ili kushikamana na maadili ya Kiisilamu na dini nyengine kama za Kikristo na imani nyengine zilizoko Zanzibar ambazo mara nyingi zinashirikishwa katika kupiga vita uvunjifu wa maadili, hasa ya Kitanzania.

Mheshimiwa kwani kuna michango ya pamoja ambayo hata vitabu vimetungwa kwa pamoja, lakini kwa mujibu wa imani vinavyotumiwa katika Jumuiya zao.

Aidha, nipongeze juhudi kwa viongozi wa Dini kama Ndugu Fadhil Soraga na wenzake katika jitihada ya kuanza kutoa elimu ya jamii kwa vijana wanawake na wanaume wanaopewa elimu ya awali ya ndoa kwa wale wasiojua vizuri, ili kupunguza suala la ndoa za utotoni na talaka ambazo zinawafanya watoto wengi kuachiwa wanawake katika ulezi. Naunga mkono programu zote zipewe fedha kama zilivyoomba ili kukamilisha mipango yake.

Mwisho napongeza utayarishaji wa sheria mbali mbali zilizorekebishwa kwa kufanyiwa kazi na ofisi yako ya wanasheria na baadaye kupitishwa na Baraza la Wawakilishi, hatimaye kutiwa saini na Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.

Sheria hizi zinazogusa jamii baada ya kadhia kadhaa hasa ya kutopewa dhamana wakosaji wa udhalilishaji. Ilikuwa itangazwe ndani ya vyombo vya habari ili kila mtu ajue lini imekamilika. Wanawake na watoto walikuwa wanangoja kuisherehekea wengi hawajui. Ahsante na ubarikiwe.

Mhe. Mwantatu Mbarak Khamis: Naomba kuwasilisha mchango wangu wa maandishi kwa Wizara ya Nchi (OR) Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Nije Fungu G06 Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Nampongeza Mhe. Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Mwanasheria Mkuu pamoja na watendaji wote wa wizara hii.

Nampongeza Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kuimarisha Mamlaka ya Utiaji wa Haki zikiwemo Mahkama. Aidha, nimpongeze Mhe. Rais tena kwa kutia saini Sheria ya Adhabu ili kuhakikisha yale makosa ambayo ni kero kubwa kwa wananchi yanapata ufumbuzi.

Mchango wangu kwa Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ofisi hii inakabiliwa na upungufu wa wafanyakazi na pia ukosefu wa wataalamu kwa baadhi ya kada kama wafamasia na wahandisi.

Kwa uzito wa ofisi ya "*CAG*", suala hili ni muhimu kupatiwa ufumbuzi ili kutekeleza vyema na kwa wakati majukumu yao. Aidha, nishauri kuna vijana tayari walishafanyiwa usaili na taratibu nyengine za uajiri kuwaajiri vijana hawa ili kupunguza changamoto ya upungufu wa wafanyakazi katika chombo hiki muhimu. Naomba kuwasilisha.

$$$

FUNGU G01 - OFISI YA RAIS KATIBA, SHERIA, UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA

Kifungu PG 0103	Programu Kuu ya Usimamizi wa Utawala Bora na Haki za Binaadam	1,046,620,000

Kifungu PG 0104

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, naendelea tu sasa hata pale katika wachangiaji katika orodha ile hukuweza kunitambua Mheshimiwa lakini katika kuniweka sawa, kuninyoosha pale kanijua sana ninamshukuru kwa hilo.

Nia yangu nafikiri haikuwa mbaya kutaja nilikotaja mimi ni mwakilishi wa Jang'ombe, sasa nilitaja vile kama nimekosea kutaja vile basi nafuta ile kauli lakini bado anakuwa mwakilishi wa jimbo lile ambalo hataki nilitaje, na ile changamoto ingekuwepo katika jimbo lile sikua na nia mbaya kusema ni pahali fulani hapana, lakini ni kero yangu ya muda mrefu sana. Mimi nimetoka Jang'ombe na Mwakilishi wa Jang'ombe kadhia ile naijua mimi niliyekuwepo pale Jang'ombe ninapofuatwa na wananchi na wale mashehe.

Mhe. Waziri kajibu tu kirahisi kwamba ah! haya mambo yashaelekea mpaka juzi Mhe. barua imetoka Wizara ya Ardhi kwamba atoe maelekezo tu kama hawa watu wapewe, imejibiwa kimtego mtego. Mhe. Katibu Mkuu kasema siko tayari kuingia katika mtego huu. Sasa kama yeye ndie mwenye masuala yale ya dini basi amwelekeze kwamba msikiti huu warudishiwe watu wa Hidayatu ili yale mazogo yaishe. Sasa naomba ufafanuzi kwa hilo na kama nimemkwaza kwa lugha yangu ile namuomba radhi. (*Makofi*)

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Katiba Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Mwenyekiti kwanza..

Mhe. Spika: Ongea na kiti tafadhali, endelea nimekupa wewe uzungumze.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Katiba Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mheshimiwa, unajua hamu ni kitu kibaya kwa sababu nimeridhika na maombi aliyoniomba radhi mwenzangu na mimi namsamehe, lakini nataka nimuhakikishie kwamba jana nimemwambia Katibu Mkuu wangu alifutilie, amuandikie barua kwamba sisi hatuna pingamizi msikiti huu kurejeshwa hati yao kwa kamati inayohusika. (*Makofi*)

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Ahsante sana nashukuru na Baraza hili la Wawakilishi ni mashahidi Mhe. Waziri katoa kauli kwamba kwa maelekezo urudishwe katika msikiti wa Hidayat. Panapo uhai bajeti ya mwaka 2019 ipo kama mambo mengine hayajakamilika ile pale imekuja tena mbele yenu muje kunisaidia. Ahsante sana tuendelee.

PG0104	Programu Kuu ya Usimamizi ya Masuala ya Kidini.	1,538,000,000
PG0105	Programu Kuu ya Uendeshaji na Uratibu	4,819,856,000

	wa Ofisi ya Rais Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora.	
PG0106	Program Kuu ya Usimamizi wa Watumishi wa Umma.	789,500,000
PG0107	Uimarishaji wa Kumbukumbu na Mawasiliano ya Serikali	715,024,000
Jumla kuu		**8,909,000,000**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

FUNGU G02 MAHKAMA KUU

PG0201	Utawala Unguja	580,710,000
PG0202	Utawala Pemba	79,200,000
Jumla Kuu		**659,910,000**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

FUNGU G02- MAHAKAMA KUU

PG0201	Programu Kuu ya Usimamizi wa Upatikanaji wa Haki	2,428,932,000
PG0202	Programu Kuu ya Uendeshaji na Uratibu wa Mahakama Kuu	

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe Mweyekiti, nakushukuru kunipa nafasi hii, lakini pia nataka nimshkuru sana Mhe. mwalimu wangu Maalim Haroun Ali Suleiman leo inaonesha kaamka vizuri. Mhe. Mwenyekiti, nilikua kwanza nataka tu nimwambie Mhe. Maalim Haroun sina haja ya kupelekwa elimu mbadala kwa sababu sikuwahi kutokea nafasi ya tano tokea darasa la kwanza mpaka nimefika *form IV*. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, kwa bahati mbaya sikupata kuendelea *form V* na *form VI*, lakini nilisoma elimu ya uatawala katika Chuo cha Utumishi wa Umma na nashukuru nilipata *certificate* ilikuwa *recommendation* kwenda *Diploma* lakini kwa bahati mbaya Diploma walikua hawajaanzisha Dar-es-Salaam nilikua sina pesa nikaishia Kwamtipura.

Mhe. Mwenyekiti nakuja katika hoja yangu, kwanza namshukuru sana Mhe. Mwanasheria Mkuu amejibu vizuri suala langu lakini kuna mambo mawili niliyazungumza, sio suala la moja kwa moja stahiki za wale mahakimu ya mahakama ya ardhi, isipokuwa Mwenyekiti wa Mahakama ya Ardhi stahiki zake zile za kupowa *post* ile *post* sio mishahara na marupurupu mengine yale wanalipwa vizuri tunashkuru *Alhamudulilah.*

Lakini unapoteuliwa ina maana kuna haki zako za uteule zile ndio ambazo nilizokuwa nazidai hapa, sasa hizi nadhani Mwanasheria Mkuu pamoja na Mhe. Waziri kama watakuwa wanafahamu hilo basi labda wanipe maelezo kama hawafahamu hilo basi hiyo hali hasili ndio ulivyo na kwasababu mimi ni Mwenyekiti wa Kamati ya Ardhi, hiyo ndio kadhia ambayo mpaka nakwenda kupitisha bajeti suala hili likikuwa halijakaa sawa. Wizara ya ardhi wanasema aaa! hili Mahakamani kwa sababu hawa ni watumishi wa Mahakama kwa hivyo, watumishi wa Mahakama hapa leo mabosi wao ndio wapo wateweza kutupa huo utaratibu.

Lakini jengine nimekuwa nilijaribu kuzungumzia la *incentive.* Sasa hivi Mhe. mambo yanabadilika kila siku sheria tunapodilisha ina maana wale mahakimu wetu inabidi tuwa-*update* sasa zinapokuwa semina na mafunzo mengine mbali mbali ambao wanashirikiana pengine wakati mwengine na wenzao wa Tanzania Bara, wale Mahakimu wa Mahakama ya Ardhi zile semina wanakuwa hawapati, kwa hivyo bado wanabakia na ile ile Taaluma waliyokuwa nayo wanakuwa hawako hawapo *updated* sasa hii ilikuwa ni *incentive.* Lakini zaidi hoja yangu ilikua katika suala zima la haki au stahiki za kupewa nasafi au za kushika nafasi za Mwenyekiti wa Mahakama ya Ardhi. Ahsante sana Mwenyekiti.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. nikushukuru na nimshukuru Mhe. Hamza kwa kutambua kama nilijibu hili suala vizuri. Nikweli na mimi nilimfahamu Mhe. Hamza alipokuwa anataka kwenda kama yeye alikuwa hana wasiwasi na kifungu 5 cha sheria ambacho kimeeleza kwamba Mwenyekiti, Naibu Mwenyekiti na Hakimu wote wapo pale mishahara na stahiki zao nyengine zote zitakuwa ni sawa na Mahakimu wa Mkoa. Huo ndio utaratibu wa kisheria ambao upo, anachosema Mhe. Hamza ni kama kwasababu na yeye umeteuwa kuwa ni mwenyekiti basi apewe na stahiki nyengine za kushika ile nafasi ya uwenyekiti.

Mimi nimwambie wenyeviti wako wengi Mhe.Mwenyekiti, sio tu hawa kwenye mahakama kuna Mwenyekiti wa *Tribunal,* Mahakama ya Biashara, kuna wa kusimamia kodi. Sasa utaratibu wa kisheria sasa hivi ulivyowekwa ni kama hawa wanabaki kuwa ni watumishi wa kimahakama wanaanzimwa kwenye taasisi nyengine. Sasa kama anataka tufanye utaratibu baina ya zile taasisi ambazo wanapelekwa kama watakuwa wanatupa labda *allowance* fulani ya kufanya kazi zao, labda hilo tuendelee kuzungumza serikalini kupitia kamati yake kujua tunaweza tukulifanyia kazi kwa namna gani.

Kwa ilivyo sasa hivi Mhe. Mwenyekiti, utaratibu wa kisheria hauruhusu hayo ambayo Mhe, Hamza ambayo ameyazungumza lakini nafahamu nini hoja yake Mhe. Mwenyekiti.

Mhe.Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, nimemfahamu sana Mhe. Mwanasheria Mkuu kama labda hatukufikia muafaka hapa naamini tutakaa shura ili kulizungumza hili. Lakini hoja yangu kwamba yule Mwenyekiti wa Mahakama yeye ndie mkuu wa mahakimu wote kwa zile Mahakama za Ardhi na ina maana hata ile bajeti ambayo inayokwenda katika mahakama ina maana yeye ndiye anayeisimamia na yeye ndiye mkuu wa utawala katika eneo lile sasa ndio maana, sio mahakimu wote wale Mahakama ya Ardhi lakini yule Mkuu wao pale ina maana ameshika *post* na ametangwazwa ameteuliwa sasa hili ndio maana nikasema Mhe. Mwenyekiti hapa tayari kuna haki inabidi zizingatiwe.

Sasa labda anipe ufafanuzi kama nilivyosema kama itakuwa bado halijakaa sawa nafikiri muda tunao kwa sababu haja yetu sio kuzuia fungu, haja yetu haki za wafanyakazi waweze kupata stahiki zao kwa mujibu wa sheria. Ahsate mwenyekiti naomba ufafanuzi.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti, ninakushukuru kama nilivyosema utaratibu huu mzima wa Mahakama ya ardhi unaongozwa na sheria na. 7 ya mwaka 1964 na kifungu cha 5 ambacho nimekieleza ndio kifungu ambacho kinaelezee utaratibu ambao upo kwa sasa hivi. Nimesema natambua hoja ya Mhe. hamza ambayo amekuja nayo na nimesema kwamba kwa utaratibu wa kisheria sasa hivi ulivyo hayo ambayo Mhe Hamza amekuja nayo hayawezi kutekelezeka kwenye *arrangement* ya sheria ambayo ipo kwa sasa hivi. Sasa inawezekana hoja yake ni ya msingi na ndio maana nikamwambia basi tukae baadae hiyo hoja yake, lakini ajue tu sio Mwenyekiti wa Ardhi na kuna wenyekiti wengine ambao wanasimamia hizi zinazoitwa *Quasi-Judicial* taasisi hizi zenye muundo wa kimahakama ambazo nao wapo wengi. Sasa sio tutizame hii halafu mwakani aje mwengine aseme na hii tumeisahau kama kutizama basi tuzitizame zote kwa jumla halafu tujue tunapendekeza nini. Lakini kwa ilivyo sasa hivi Mhe. Mwenyekiti utaratibu wa kisheria hauruhusu kufanya haya ambayo Mhe. Hamza anayapendekeza Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti: Labda nafikiri ungekwenda zaidi kidogo kwa sababu hoja ya Mhe. pamoja na kuwa sheria hairuhusu iko *valid* kwa sababu inagusa haki za wale ambao wako katika hizo sehemu. Pamoja na hao wengine ambao wewe umewataja sasa labda uahidi hapa mbele ya Baraza kwa sababu umeulizwa humu ndani uahidi hapa hapa kwamba hili suala mtalifinyia kazi na mtashirikiana nao baadhi ya hao waheshimiwa ambao wanaliona hili ili kutafuta namna nzuri zaidi ya kwenda kuliweka sawa hili suala.

Mhe. Mwanasheia Mkuu: Mhe. Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kutaka ufafanuzi zaidi, kama nilivyosema haki zake mshahara na stahiki ambazo wanapata mahakimu wote ambao wapo sasa hivi ndio hawa wanatakiwa wapate sawa sawa, hizo ndio haki wanazotakiwa hawa wapate. Kama alivyosema Mhe. Hamza kama yeye hana tatizo na haki hizo za mishahara na hayo maposho mengine ambayo wanapewa mahakimu na mwenyekiti wa ardhi na naibu wake na hakimu aliyekuwa pale na anapata hizo hizo.

Hoja ya Mhe. Hamza ni kama mbali ya hapa ile *top up* ya kwa sababu tu ya yeye mwenyekiti ndio anataka iwepo kwa mwenyekiti wa ardhi, ninachoweza kusema Mhe. Mwenyekiti ni kwamba ninalichukua tutakwenda kulitazama pamoja na wale wengine ambao wanaongoza taasisi hizi zenye kimfumo wa Mahkama ili kujua tunalitazama vipi kwa jumla mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Spika: Mhe Hamza nadhani tumefika pahali, ahsante naomba tuendelee.

PG020 Programu Kuu ya Uendeshaji na Uratibu wa Mahakama Kuu	4,296,568,000
Jumla Kuu	**6,725,200,000**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya

mabadiliko yoyote)

G035 MWANASHERIA MKUU ZANZIBAR

FUNGU - G03 MWANASHERIA MKUU ZANZIBAR

PG0301	Programu Kuu ya Mageuzi ya Utoaji Huduma za Sheria	932,825,000

Mhe. Shehe Hamad Matar: Mhe. Mwenyekiti, sina nia ya kuzuia lakini nilitaka nipate maelezo kuhusu mambo mawili katika ofisi ya Mwanasheria Mkuu, katika mchango wangu niliomba kwamba Mwanasheria Mkuu Ofisi yake iweze kuleta sheria ambayo kuwa tumeipitisha ambayo kuwa inalalamikiwa na wananchi na sisi ni wawakilishi wa wananachi kuhusu sheria ya kiinua mgongo ya ZSSF, yawe tayari kuona kwamba ile sheria ina manung'uniko mengi yeye hayuko tayari kuileta hapa kuweza kufanya marekebisho. Lakini pia vile vile suala zima la kamati ya bajeti kupata sheria suala hili hakulieleza katika majibu yake, naomba sana kupata majibu ya maelezo haya.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Ni kweli na nimuombe radhi Mhe. Matar kwa sababu ya muda sikuweza kufafanua hizo hoja zake. Moja nianze na hili suala la ZSSF marekebisho ambayo tuliyapitisha ambayo ilibadilisha ile *formula* ya malipo kwa wastaafu. Nikubaliane nae kwamba ni kweli baada ya kuanza kutumika kwa sheria ile kumeonekana kuna manung'uniko mengi kutoka kwa wastaafu. agizo ambalo limetoka serikalini ni kwamba tuitazame tena ile *arrangement* ambayo ipo halafu ZSSF waje na mapendekezo yao tena serikalini, kwa hiyo linafanyiwa kazi Mhe. Mwenyekiti.

La pili alisema kamati ya Bajeti haipo kisheria *of cause* sasa hivi Kamati ya Bajeti inaongozwa kwenye kanuni na kanuni hizi za Baraza zimetungwa na ile sheria ya Baraza na. 4 ya mwaka 2007. lakini hoja kama anayo bado tunayo nafasi katika sheria yetu ya utawala wa Baraza na kuweza kutizama namna gani tunaweza tukaya-*commodate* haya mambo mengine ambayo yanakiwa yawemo kwenye ile sheria ya Utawala wa Baraza. Kwa hivyo hoja zake mbili zote utaratibu wake upo na utafanyiwa kazi Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Shehe Hamad Matari: Mhe. Mwenyekiti tuendelee.

PG0301	Programu Kuu ya Mageuzi ya Utoaji wa Huduma za Sheria	932,825,000
PG0302	Programu Kuu ya Uendeshaji na Uratibu wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu	1,094,575,000
Jumla Kuu		**2,027,400,000**

FUNGU G04 - OFISI YA MKURUGENZI WA MASHTAKA

Kifungu PG 0401

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, wakati jana nilipokuwa nachangia nilichangia namna malalamiko niliyotoa juu ya ucheleweshwaji wa majalada kutoka kwenye Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka kwenda Mahakamani. Inachukua pale pana kesi zaidi ya miaka miwili, miaka miwili na nusu wananchi wetu wanasikitika japo kama wametenda makosa, lakini wapelekwe kule kunakopatikana au kule kunakotafsiriwa sheria ili waweze kupata haki zao. Lakini kila siku nenda rudi upelelezi bado au namna gani, kwa hivyo ina changamoto kubwa sana.

Je, tatizo ni nini mpaka inapelekea haya nafikiri Mhe. Waziri aje anipae ufafanuzi wake.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Nakushukuru Mhe. Mwenyekiti, *of course* na suala la Mhe. Diwani hakuja na takwimu ili Baraza likajua vizuri, kwenye majalada hayo ambayo yanapelekwa Ofisi ya *DPP* mangapi, kwa hivyo hakuja na takwimu kwa hivyo inakuwa vigumu kumjibu suala hilo. Lakini kimsingi Ofisi ya *DPP* inafanyakazi zake vizuri na sasa hivi wana mashirikiano mazuri na polisi lakini niseme kama Ofisi ya *DPP* kwa mujibu wa katiba yeye ndio amekabidhiwa kufungua mashtaka, lakini sio kila jalada linalopelekwa kwake na yeye analipeleka Mahakamani kabla ya kulisoma, na yeye inabidi asome ajiridhishe na kama kuna mapungufu katika ushahidi ambao umeletwa na polisi, ana wajibu wa kulirudisha jalada lile na kuwaagiza polisi kufanya marekebisho.

Sasa utaratibu wake ni mkubwa kidogo, lakini nimuhakikishie kama nilivyosema, kwamba wenzetu Mahakama wameanza kuja na ile *secular* ambayo sasa imetoa utaratibu mzima wa kuanza kusikiliza kesi mpaka kumaliza na sisi kwenye taasisi zetu nyengine tuna wajibu wa kufuata utaratibu huo, wa kuhakikisha tunajiwekea muda wa mafaili haya yanayoingia maofisini kwetu na kuyatoa ili aweze kuyashughulikia. Sasa hili nadhani *DPP* anafanyakazi zake vizuri, kama kuna changamoto ni hizo za kiutendaji, lakini sio za kiuzembe katika kutimiza majukumu yake. Nakushukuru Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, sipingani na Mhe. Mwanasheria Mkuu kwamba Ofisi ya *DPP* haifanyi kazi vizuri, inafanya kazi vizuri asilimia 95 haina shida katika hilo. Lakini hoja yangu ilikuwa katika haya majalada ambayo tayari yako pale yana zaidi ya mwaka, nyingi inaanzia mbili, tatu na kuendelea. Sina takwimu nyingi ya ngapi, lakini mbili inaanzia tatu, nne na kuendelea. Hata kwenye kitabu chao utaona mpaka dakika hii kesi ambayo Mahakama Kuu ni moja tu mwaka mzima ambayo iliyotolewa maamuzi, pamoja na kadhia nyingi sana za kesi zilizokuwepo pale.

Mhe. Mwenyekiti, mimi mwenyewe nina kesi mbili ambazo mpaka dakika hii nazifuatilia. Moja yule kijana wangu aliyefanyiwa vibaya kule Jang'ombe mpaka leo maamuzi bado, sasa hata jalada lake linaambiwa bado *DPP* hajakamilisha. Kwa hivyo, lazima tukiona kama hivi na sisi ndio wasemaji wa wananchi tuwasemee katika hayo na hatuna pakwenda kuyasema hayo isipokuwa ni humu ndani. Sasa ningeomba tu Mhe. Mwanasheria Mkuu kwamba hili suala alikubali, akae na watu wake afanye utaratibu ili haya mambo yaende haraka ili tuone watu wetu wanapata haki zao za msingi.

Mhe. Mwenyekiti, sina nia ya kuzuia fungu, lakini nia yangu ni kuishindikiza serikali kwamba isimamie utaratibu ili kesi ziende haraka, huu msongamamo wa nenda rudi panda shuka umalizike. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru najua Mhe. Abdalla Maulid Diwani alivyosema kesi zisikilizwe kwa haraka, alikuwa anakusudia kusema kifungu cha 12(6)(e) cha katiba ambacho nilikisoma, kwamba katiba inaweka sharti na kesi jinai kusikilizwa na hukumu yake kutolewa kwa haraka. Kwa hivyo, ofisi zetu zote hizi Mhe. Mwenyekiti, niliahidi Baraza lako kwamba tutaendelea kufuata masharti ya kifungu hicho, ili tuhakikishe haki zinatolewa kwa haraka. Kwa sababu usemi wa kisheria maarufu wote wanaujua kuwa, *"Justice delayed is justice denied"*. Kwa hivyo, hatutokuwa kwenye nafasi ha kuhakikisha tunaichelewesha haki kwa sababu tu ya taratibu nyengine ambazo sio za kisheria. Nakushukuru Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Tuendelee Mhe. Mwenyekiti.

Kifungu PG 0401	Programu Kuu ya Uendeshaji na Usimamizi wa Kesi za Jinai	615,753,000
Kifungu PG 0402	Programu Kuu ya Uendeshaji na Uratibu wa Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka	2,089,347,000
	Jumla Kuu	**2,705,100,000**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya Mabadiliko yoyote)

FUNGU G 05 - TUME YA KUREKEBISHA SHERIA

Kifungu PG 0501	Programu Kuu ya Kufanya Mapitio ya Sheria	674, 770,000
Kifungu PG 0502	Programu Kuu ya Utawala na Uratibu wa Kupitia Sheria	370,430,000
	Jumla Kuu	**1,045,200,000**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya Mabadiliko yoyote)

FUNGU G 06 - OFISI YA MDHIBITI NA MKAGUZI WA HESABU ZA SERIKALI

Kifungu PG 0601	Utawala Unguja	50,954,000

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa tena nafasi hii nikapata ufafanuzi wa ziada. Kwanza namshukuru sana Mhe. Waziri kwa yale majibu aliyokusudia kujibu kwa kweli kayajibu vizuri sana. Lakini nilikuwa nataka nyongeza tu ili tuweze kwenda vizuri.

Mhe. Mwenyekiti, nazungumzia suala la wafanyakazi ambao walihamishwa. Sisi wajumbe sote tunajua kwamba

Mhe. Mwenyekiti: Bado, tuko kwenye mapato.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Si utawala kasema.

Waheshimiwa Wajumbe: Hapana, bado.

Mhe. Mwenyekiti: Kwenye matumizi. Tuendelee.

Kifungu PG 0601	Utawala Unguja	50,954,000
	Jumla Kuu	**50,954,000**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya Mabadiliko yoyote)

FUNGU G 06 - OFISI YA MDHIBITI NA MKAGUZI WA HESABU ZA SERIKALI

Kifungu PG 0601	Programu Kuu ya Udhibiti wa Fedha na Rasilimali za Umma	1,354,813,000

Kifungu PG 0602

Mhe. Mwenyekiti: Haya, nitampa Mhe. Hamza Hassan Juma, atafuatiwa na Mhe. Abdalla Maulid Diwani na Mhe. Omar Seif Abeid hilo jambo lako utalisema. Mhe. Hamza Hassan Juma anza.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa tena hii nafasi. Mhe. Mwenyekiti, hoja yangu hapa nilikuwa nimejaribu kueleza kuwa tunafahamu kwamba Ofisi ya Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali ni ofisi nyeti sana katika nchi zote duniani, na ofisi hii tunavyofahamu ina upungufu mkubwa wa wafanyakazi, yaani watumishi na kazi zao kwa kweli ni kazi ambazo zinatusaidia sisi Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kuweza kupata taarifa sahihi hasa za matumizi katika taasisi zetu mbali mbali za serikali. Sasa kadhia iliyokuwepo ofisi ina uhaba wa watumishi, lakini ofisi hiyo hiyo tayari imetoa uhamisho kwa watumishi. Kwa hivyo, ina maana zile nafasi ambazo walikuwa wanafayakazi wale sasa hivi ziko tupu, wafanyakazi wale wamepelekwa sehemu nyengine. Wakati mwengine *CAG* anaajiri, samahani. Anaomba au unaweza kusema sijui kizungu ndio ku-*hire*, lakini kama ana kodi vile ili waje wamsaidie zile kazi.

Mhe. Mwenyekiti, hapa ndio kidogo inavyotupa mashaka. Sasa aidha, kama pengine kuna kutowajibika vizuri, basi angalau tungeona kwamba mtu kapewa barua ya onyo kwamba kitu anachokifanya sicho. Lakini sasa kama mtu anahamishwa pale pana-*vacant*, mimi nafikiri sio utaratibu. Sasa hili kidogo Mhe. Waziri alilitolea ufafanuzi akasema uhamisho ni suala la kawaida. Sawa ni suala la kawaida, lakini pahala ambapo pamejaa na hii itakuwa ni sawa sawa

na waheshimiwa waliozungumzia ugatuzi Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali. Walimu wanahamishwa katika skuli wanakwenda sehemu nyengine hawana kazi ya kufanya, pale walipoondoka walimu hakuna. Kwa hivyo, na hili litakuwa ni sawa sawa na Ofisi ya *CAG* kidogo tunataka ufafanuzi, ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Waziri wa Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Mwenyekiti, namshukuru sana Mhe. Hamza Hassan Juma, asisahau tu kwamba na mimi nakumbuka vile vile jinsi alivyokuwa anawanyanyasa wanafunzi wenzake kwa uhodari. Kwa hivyo, asiwe na mashaka nakumbuka vizuri umakini wake na umahiri wake.

Mhe. Mwenyekiti, nimesema mwanzo hapa na katika maelezo yangu ya *CAG* nashukuru sana, kwamba *CAG* alikuwa kakwama kwa upande fulani kuwaajiri wafanyakazi wapya, kwa sababu bodi ilikuwa haipo kisheria na hii ni Wizara ya Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora, ni lazima tufuate taratibu za kisheria. Nilisema hapa kwamba sasa hivi Mhe. Rais ameshamteuwa Mwenyekiti, na kazi iliyobakia ni waziri kuteuwa wajumbe. Mhe. Mwenyekiti, napenda niwahakikishie kwamba *CAG* alikuwa keshafanya kazi nzuri sana, yaani tayari keshafanya mpaka *interview* kwa wale wafanyakazi ambao atawachukua na watakaokidhi mahitaji ya ofisi yake.

Mhe. Mwenyekiti, lakini hili suala la kwamba inabidi akodi hawa *hire services.* Huu ni utaratibu wa kawaida kimataifa, kama hana mtaalamu wa mambo ya *engineering* ana mambo ya mazingira basi ni lazima ata-*hire services* madamu ni watumishi tu basi kazi inaweza ikenda. Kwa hivyo, ni utaratibu wa kawaida.

Mhe. Mwenyekiti, napenda niwahakikishie Waheshimiwa Wajumbe, kwamba watulie siku sio nyingi katika kipindi cha wiki moja, mbili au tatu Inshaallah Ofisi ya *CAG* itakuwa na wafanyakazi wa kutosha kwa mujibu wa utaratibu na mahitaji yake tukijaaliwa.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, mimi najua Mhe. Waziri mwalimu wangu, ananijibu kiuwalimu. Mhe. Mwenyekiti, unapowahamisha wafanyakazi wenye *experience* unakwenda kuwaajiri *fresh from collage,* ofisi nzito kama hii Mhe. Mwenyekiti, hilo ni tatizo. Kwa sababu hawa hata wakisha ajiriwa itabidi kwanza wakae wajifunze *on job training*.

Mhe. Mwenyekiti, kwa nini alikuwa asisubiri aajiri halafu ndio baadae aweze kufanya uhamisho. Mhe. Mwenyekiti, sote tunajua katika kitu cha mahesabu. Sisi wenyewe Waheshimiwa Wawakilishi, mtu anapoteuliwa Kamati ya *PAC,* kwanza inabidi ndani ya kipindi cha mwanzo lazima apate mafunzo ya kutosha ili kuweza kuangalia. Sasa leo Mhe. Mwenyekiti, hapa kuna tatizo.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nafikiri labda Mhe. Waziri ili nisiendelee kuzozana nae sana, mimi nafikiri hebu aliangalie upya. Najua Ofisi ya *CAG* kwa mujibu wa katiba ina-*immunity* yake haipendi kuingiliwa, lakini katika masuala ya utawala Mhe. Mwenyekiti, hebu naomba Mhe. Waziri hili hapa kuna jambo, hebu naomba twendeni *deep*. Kuondoa mtu mwenye *experience* ukamleta *newcomer* katika ofisi nzito kama hii.

Mhe. Mwenyekiti, leo tunadai ripoti za miaka mingapi. PAC kuna ripoti tatu bado, sasa hapa kuna kazi kubwa ya kufanya. Mimi nafikiri Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri tu mimi nimuombe, maana yake sitaki nisimame tena katika hili. Kwa hivyo, nimuombe alifanyie kazi kwa njia ambazo zinazostahiki, lakini bado mimi nataka kusema hapa kuna tatizo. Ahsante sana, sasa anijibu tu kwamba atalifanyia kazi kwa njia ambazo atakazozijua yeye, kwa kuwa ofisi ya *CAG* ina *immunity* basi ili tupate kuendelea. Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Waziri wa Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Mwenyekiti, litafanyiwa kazi kwa mujibu wa sheria na suala hili nitalikabidhi kwenye bodi tukijaaliwa watalifanyia kazi kwa mashauriano ya karibu kabisa kati yake yeye na wizara hii.

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, nafikiri Mhe. Hamza Hassan Juma kanikopia kichwa changu, kwa hivyo wacha tuendelee kesi yangu ndio hiyo hiyo.

Mhe. Omar Seif Abeid: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi. Mhe. Mwenyekiti, nilipokuwa nikichangia jana nilionesha nia ya kuhoji kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwenye mambo mawili.

Jambo la kwanza nilitaka kujua ni lini tutapatiwa ripoti ya mradi ule wa mkonga wa taifa na wa pili wa viwanja vile vya Kariakoo vile ambavyo viko chini. Lakini pia Mhe. Mwenyekiti, nilitaka nijuwe, niliulizia. Tumepokea ripoti mara mbili ya Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusu udhibiti wa fedha za umma, kwamba wako hata watu ambao walitajwa kwenye ripoti ile, nilitaka nijuwe ni hatua gani zilichukuliwa baada ya wale watu kutajwa kwenye ripoti ile na zile taasisi ambazo zimepata hati chafu. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Waziri wa Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Omar Seif Abeid na yeye ni mwanafunzi wangu vile vile huyu, afanye subira. CAG anafanyakazi kwa mujibu wa katiba ya nchi, na zitakapokuwa tayari ripoti zote, iwe za miradi ya maendeleo na za taasisi nyengine zote zitaletwa hapa kwa utaratibu wa kawaida. Kwa hivyo, afanye subira tu *Inshaallah* tutalifanyia kazi hili.

Mhe. Omar Seif Abeid: Tuendelee Mhe. Mwenyekiti.

Kifungu PG 0602	Programu Kuu ya Utawala na Uendeshaji wa Udhibiti na Ukaguzi Mkuu wa Hesabu	1,667,387,000
	Jumla Kuu	**3,022,200,000**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya Mabadiliko yoyote)

FUNGU G 07 - MAMLAKA YA KUZUIA RUSHWA NA UHUJUMU WA UCHUMI

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe, taratibuni kidogo. Hansard siku hizi ina matatizo kidogo, kwa hivyo mkifanya zogo kidogo hawapati. Tuendelee.

Kifungu PG 0701 Programu Kuu ya Kupunguza Vitendo

Mhe. Dkt. Mwinyihaji Makame Mwadini: Mhe. Mwenyekiti, sina azma ya kuzuia fungu la Mhe. Waziri, nina ushauri tu, hili suala tumeshalizungumza mara nyingi lakini naona bado linajirejea na hakuna maendeleo yoyote.

Mhe. Mwenyekiti, Ofisi hii inafanyakazi nzuri sana ya kuleta hizi kesi za tuhuma ya wahujumu uchumi, karipoti mwenyewe 151 zimepatikana, *DPP* 39 zimefikishwa kwa *DPP*, 5 tu, ndio ziko zimefunguliwa majalada Mahakama Kuu.

Mhe. Mwenyekiti, Kwanini 5 zimefunguliwa,yaani hakuna hata kesi moja iliyofanyika isi-*conclusive* tatizo nini, nishawahi kumuomba sana Mhe. hili suala, kama kunatatizo sheria hii basi bora ilete afanye marekebisho lakini kesi hazendi kwa nini. *(Makofi)*

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti, nadhani ufafanuzi ambao niliutoa awali kuhusiana na utaratibu mzima wa kusikiliza kesi hizi kutoka Ofisi ya *DPP* kwenda Mahkama *of course*, ndio huo huo unachukua pia na huu wa Mamlaka ya Rushwa na Uhujumu wa Uchumi. Kwa hivyo, tutajitahidi kutekeleza yale masharti niliyoyaeleza kwenye Katiba na kuhakikisha tunasisumamia vizuri majukumu haya. Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Dkt. Mwinyihaji Makame Mwadini: Mhe. Mwenyekiti, sina tatizo. Ushauri nimeutoa na Mhe. Mwanasheria Mkuu kaukubali, tuufanyie kazi tu Mhe. Mwenyekiti. Ahsante.

Kifungu PG 0701	Programu Kuu ya Kupunguza Vitendo vya Rushwa na Uhujumu wa Uchumi	320,850,000
Kifungu PG0702	Programu Kuu ya Uendeshaji na Uratibu wa Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu wa Uchumi	**1,269,950,000**
	Jumla Kuu	**1,590,800,000**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

FUNGU G 08 – KAMISHENI YA UTUMISHI WA UMMA

Kifungu PG 0801 Programu Kuu Usimamizi wa Utumishi wa Umma

Mhe. Shehe Hamad Mattar: Mhe. Mwenyekiti, nilipokuwa nikichangia nilimuuliza Mhe. Waziri kuhusu kadhia ya Wasaidizi Wahasibu Wakuu Pemba, hadi leo kupata mafao yao na jambo hili lipo katika ofisi yake. Je, wamefikia wapi katika kuweza kupata haki yao?

Mhe. Mwenyekiti, vile vile suala la usafiri ambapo mwaka jana tulilileta wakasema wataliangalia, la wafanyakazi waliokuwa mikoa miwili ya Kaskazini na Kusini Pemba, kupatiwa usafiri wa kwenda na kurudi kazini ili kuweza kuwahi kazini. Mwaka jana walisema suala hili watalishughulikia watalichukua Jee, sikupata maelezo.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kupata maelezo.

Mhe. Waziri wa Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Mwenyekiti, swali hili la pili la usafiri mimi sikumfahamu anavyokusudia. Anahitaji wale wafanyakazi kila mmoja tumpatie usafiri au anahitajia jambo gani, anisaidie kidogo ili niweze kumjibu vizuri zaidi.

Mhe. Shehe Hamad Mattar: Ahsante Mhe. Mwenyekiti. Nilikusudia uwepo usafiri wa pamoja, usafiri unaotoka kama Wete kwenda Chake na Chake kwenda Mkoani na kurudi hapo wafanyakazi kidogo waweze kupata unafuu wa safari na kufika kazini kwa wakati na kuondoka. Huo ndio kusududio sio kila mmoja kupatiwa wake, kama vile Mikoa myengine inavyofanya hapa ipo na usafiri unakwenda Kaskazini baadae wafanyakazi wanarudishwa. Ahsante Mwenyekiti.

Mhe. Waziri wa Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Mwenyekiti itakuwa vyema wakipatiwa usafiri lakini tatizo ni suala la Kamisheni yenyewe kufanya utaratibu huo sasa wao. Sasa wao hatuna matatizo kila mmjoa, hata hapa Barazani tulipo Baraza lina basi lao. Na Taasisi yenyewe ifanye jitihada hizo za kutafuta, tutajitahidi kushirikiana kuwaelekeza kwamba watafute utaratibu wa kutafutia usafiri basi. *(Makofi)*

Mhe. Shehe Hamad Mattar: Mhe. Mwenyekiti, suala la pili hajalitolea maelezo wafanyakazi, haki za wafanyakazi wasaidizi wahasibu, hajalitolea maelezo.

Mhe. Waziri wa Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Mwenyekiti, sisi Wizara yetu inachukua maamuzi baada ya kutoa maamuzi baada ya maombi kutoka wizara husika, au sekta husika. Kwa hivyo kama kuna malalamiko yote ya wafanyakazi, sekta husika watuletee na sisi tunaahidi kwamba tutazichykulia hatua. *(Makofi)*

Mhe Mwenyekiti: Umeridhika Mhe. Shehe Hamad Mattar.

Mhe. Shehe Hamad Mattar: Mhe. Mwenyekiti, Tayari Wizara ya Fedha tayari nimeshaipelekea kupata maombi hayo. Wizara ya Fedha ishalikubali kwa ujumla wao, malalamiko hayo na ikawapelekea Ofisi yake lakini hadi leo haujatoka uamuzi hilo ndilo ninalo lisimamia mimi.

Mhe. Waziri wa Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Mwenyekiti, Bajeti hizi zipo kwenye Taasisi zenyewe, sasa ni vizuri nadhani akalifutilia vizuri Mhe. Shehe Hamad Mattar sisi tuko tayari kushirikiana na yeye Taasisi husika Wizara ya Fedha wanatoa fedha lakini taasisi zenyewe ndio zinazosimamia, na zinapanga bajeti, zinapanga kila kitu, sasa wao wanajua watumishi wao waliokwisha walipa na wale ambao hawajalipwa. Kwa hivyo mimi namuahidi tu kwamba tutashirikiana nae aje anambie maeneo gani tutazishughulika hizo Taasisi zinazohusika ili tuzikumbushe kufanya wajibu wao.

Mhe. Shehe Hamad Mattar: Mhe. Mwenyekiti, nimeridhika na nitashirikiana nae.*(Makofi)*

Jumla kuu ya Program kuu hii ni 363,818,000

Kifungu CG 0802	Program Kuu ya Uendeshaji na uratibu wa Kamisheni ya Utumishi wa Umma	**671,182,000**
	Jumla Kuu	**1,133,000,000**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

G09 TUME YA UTUMISHI SERIKALINI

Kifungu PG0901	Program Kuu ya Usimamizi wa Watumishi Serikalini	228,900,000
Kifungu PG0902	Program Kuu ya Uendeshaji na Uratibu Wizara ya Utumishi	

Mhe. Hamza Hassan Juma : Mhe. Mwenyekiti, nilipokuwa nikichangia nielezea suala zima la stahiki za wafanyakazi mbali mbali hasa kutoka katika Mashirika ya Serikali**.**

Mhe. Mwenyekiti, tunajua Shirika yanavyofanya kazi, utendaji wao kidogo unatafautiana na Maidara. Sasa kuna mapendekezo mengi ya maslahi ya watumishi na hasa baada ya mabadiliko mbali mbali ya serikali kuhusu masuala ya mishahara, lakini kwa kweli bado yanachelewa sana yanafika karibu zaidi ya mwaka mzima yanakuwa hayajapata ufumbuzi.

Mhe. Mwenyekiti, Kwa hiyo, hii inapelekea vile vile baadae watu kuja kulipwa *areas* ambalo linakuwa ni usumbufu kwa upande wa serikali. Sasa hili ungelijaribu kulizungumza kwamba hii Idara ya Utawala na Uendeshaji, kwa kweli suala zima, labda niseme tu labda mfano wafanyakazi wa Shiriki la Meli, Shirika la Bandari ilikuwa ni hivyo hivyo lakini shirika la Bandari liko tayari, lakini Shirika la Meli mpaka sasa hivi bado kuhusu suala la maslahi yao halijakaa sawa. Sasa hili labda nilikuwa naomba sana Mhe. Waziri ajaribu kunipa ufafanuzi kama atakuwa na taarifa nalo kama hana basi ninafikiri ajue kwamba moja katika changamoto ya mashirika ni hiyo. Lakini hii ni moja tu, lakini kuna mashirika kama Shirika la Umeme vile vile kuna tatizo. Kimsingi mashirika ya serikali. Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Waziri wa Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Mwenyekiti, nataka nimsaidie mwanafunzi wangu kwamba masuala ya mashirika yote yako kwenye Kamisheni ya Utumishi na tumeshapita. Sasa lakini kwa faida yake namuomba baadae tukimaliza kikao mimi nitamuelekeza kwenye Kamisheni ya Utumishi wa Umma ili tuweze kulifanyia kazi, kwa sababu tumeshapita.*(Makofi)*

Mhe. Hamza Hassan Juma: Unajua Mhe. Mwenyekiti, mimi na Maalim Haroun Ali tunaelewana na kwa sababu hoja ilikuwa ili ajuwe ni eneo gani nataka kulifanyia kazi. Lakini nafikiri ameshanielewa na kama alivyosema tutakaa baadae, ili kuhakikisha kwamba hizi haki za wafanyakazi, kwa sababu kuna suala la kuzuia fungu lakini vile vile kuwakilisha yale mahitaji ya wananchi. Nafikiri tutaelewana tukitoka hapa, ahsante.

Kifungu PG0902	Programu Kuu ya Uendeshaji na Uratibu wa Wizara ya Utumishi wa Umma	**3,300,000**
	Jumla Kuu	**529,200,000**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

(Baraza lilirudia)

Mhe. Waziri wa Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Spika, ilivyokuwa Kamati ya Matumizi imejadili na kupitisha Makadirio ya Fedha na Wizara yangu bila ya mabadiliko. Sasa naomba kutoa hoja kwamba Baraza liyakubali makadirio hayo.

Mhe. Waziri wa Biashara na Viwanda: Mhe. Spika, naafiki.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, naomba sasa niwahoji. Wale wote wanaokubaliana na Mhe. Waziri kwa hoja aliyoitoa wanyanyuwe mikono. Wanaokataa, waliokubali wameshinda. *(Makofi)*

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwe na kuafikiwa)

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, naomba nichukuwe nafasi hii kumpongeza sana Mhe. Waziri na kuwapongezeni na nyinyi Waheshimiwa Wajumbe, kwa michango yenu lakini hatimaye tumeweza kuihitimisha na kuipitisha hii hoja. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wajumbe, hoja inayofuata ya Mhe. Waziri wa Habari, Utalii na Mambo ya Kale itaanza siku ya Jumatatu, japo ameshawasilisha iko kwenye *Order Paper* na tayari tuna orodha ya watu ambao wameshaomba kuichangia hiyo hoja. *(Makofi)*

Ndio Waheshimiwa Wajumbe, ni sahihi kwa sababu ikiwekwa mezani tayari unaweza ukaiandikia kuiombea. Kwa hivyo, hawa wamefuata kanuni na wamepokelewa. Kikawaida nimezoea kupokea kutoka kwa Mhe. Ali Suleiman Ali Shihata, lakini yeye hayumo katika hao. *(Makofi/Vicheko)*

Baada ya hapo Waheshimiwa Wajumbe, naomba nitoe matangazo machache ambayo yametufikia hapa. Kwanza kabisa Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali anapenda kuwakumbusha Waheshimiwa Wawakilishi wote kuhudhuria katika shughuli rasmi ya uzinduzi wa utoaji ruzuku kwa skuli za sekondari za serikali itakayofanyika kesho katika Ukumbi wa Idrissa Abdulwakil ambao ndio ukumbi wa Baraza la Wawakilishi la zamani, kama mnavyojua tayari umeshapewa jina rasmi, ni Ukumbi wa Mhe. Dkt. Idrissa Abdulwakil. Kesho Jumamosi tarehe 19/05/2018 mgeni rasmi ni Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wajumbe, wageni wetu wa leo, wa kwanza ni mgeni wa Dkt. Mwinyihaji Makame Mwakilishi wa Dimani. Wageni wenyewe ni Mr. Darling Obden, *you can raise up you can acknowledge your present, thank you. (Makofi)*

Mr. Shawal Pillati, Mr. Richard Hallas and Mr. Zaid Isaacs. Hawa ni wawekezaji kutoka Afrika ya Kusini ambao wanajishughulisha na kazi za ukulima kwa maji *Solis Hydrofarm* na maji kwa kutumia mionzi ya jua yaani *zero mass water*. *Thank you*, *you are most welcome*. *(Makofi)*

Mgeni mwengine ni mgeni wa Mhe. Omar Seif Abeid Mwakilishi wa wananchi Jimbo la Konde, mgeni mwenyewe ni bwana Abdul Mohamed kutoka Dar es Salaam, karibu sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wajumbe, baada ya matangazo hayo, naomba sasa nichukuwe nafasi hii kwa sababu bado tuna muda mwingi lakini haumtoshi Mhe. Waziri wa Habari, Utalii na Mambo ya Kale kama nilivyosema kuwasilisha hoja yake. Kwa hivyo, niakhirishe shughuli za Baraza mpaka siku ya Jumatatu saa 3:00 za asubuhi.

(Saa 5:00 asubuhi Baraza liliahirishwa mpaka tarehe 21/05/2018 saa 3:00 za asubuhi)